SportPesa
TZS. 861,636,800
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Simu** za Mbowe, Bwire zapokewa kielelezo mahakamani

UKURASA 3




UKURASA 23

Nipashe
Jumatano Januari 19, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580830
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
om/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Mbivu, mbichi U-Spika CCM

• **Kitendawili** wagombea kuteguliwa leo, chekecheo kuchuja waombaji 71 hadi watatu... *Endelea ukurasa 2*




## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**ZIMAMOTO YASEMA ILICHELEWA KUPATA TAARIFA MOTO KARUME**
JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala, limesema taarifa za kuungua...

UKURASA WA 4
**11 KUGOMBEA UENYEKITI, MAKAMU ACT-WAZALENDO**
WANACHAMA 11 wa Chama cha ACT-Wazalendo, wametia nia ya kugombea...

UKURASA WA 5
**TTB, AZAM ZAKUBALIANA KUTANGAZA UTALII**
BODI ya Utalii Tanzania (TTB) na kampuni ya Azam Media zimetia saini...

## Sugu sasa apigia debe Watanzania chanjo ya corona

UKURASA 3

## Mkewe Sabaya: Nitahakikisha mume wangu anakuwa huru

UKURASA 2

MICHEZO **PABLO AMCHAMBUA BOCCO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (kushoto) na wenzake wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, walipowasili katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kusikiliza mashtaka ya ugaidi yanayowakabili. Habari Uk. 03. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbivu, mbichi U-spika CCM

**Na Maulid Mmbaga**

MBIVU na mbichi ya wateule watatu watakaopitishwa kwa kupigiwa kura na wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa nafasi ya Spika wa Bunge, itajulikana leo.

Mchakato huo unaendelea pia kwenye Chama cha ADC ambacho ni kati ya vyama vya upinzani chenye mgombea, Maimuna Kassim, aliyejitokeza kuchukua fomu ya kuwania kiti hicho kilichoachwa wazi.

Wateule ndani ya CCM watajulikana baada ya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya chama hicho kupitisha majina matatu yatakayopelekwa kwa hatua zaidi.

Kamati hiyo iliyokutana jana na leo ndiyo inayokamilisha mchakato huo baada ya kupokea majina yaliyopitiwa na sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho.

Sekretarieti hiyo ilikutana Januari 17, mwaka huu, kujadili na kuishauri Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa wagombea waliojitokeza kuomba kiti hicho.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa awali Januari 9, mwaka huu na Katibu Idara ya Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamdu Shaka, urejeshaji fomu ulikamilika Januari 15, mwaka huu.

Kabla ya kupigiwa kura na wabunge wote, Janauri 21 hadi 30 (wiki ijayo) kikao cha chama cha wabunge wa CCM (caucus), kitapiga kura kumpata mgombea ambaye atakwenda kuomba kura bungeni.

Hadi sasa wanachama wa CCM 71 wameomba kuteuliwa na chama hicho kugombea nafasi hiyo ya u-Spika.

Miongoni mwa waliojitokeza kwenye kijany'anyiro hicho ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa UWT Taifa, Sophia Simba na aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mbunge wa Jimbo la Bariadi (CCM) kwa muda mrefu, Andrew Chenge.

Makada wengine waliojitokeza kuwania nafasi hiyo ni wabunge mbalimbali akiwamo Joseph Kasheku maarufu Msukuma, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Bunge la Afrika (PAP) na Mbunge wa Shinyanga Mjini, Steven Masele na mwingine ni msomi aliyejinasibu ana shahada tisa, Baraka Byabato.

Baada ya kukamilika kwa mchakato ndani ya chama hicho, jina litakalopitishwa litawasilishwa bungeni Februari mosi, mwaka huu, kwa ajili ya wabunge kuchagua Spika atakayepigiwa kura kushika nafasi hiyo.

Vile vile, mgombea huyo atakayepitishwa na CCM atashindana na wagombea wa vyama vingine kwa wingi wa kura za wabunge baada ya kujinadi mbele yao wakati wa vikao vya bunge.

Mchakato wa kumpata Spika mpya umeanza baada ya Spika Job Ndugai kujiuzulu nafasi hiyo Januari 6, mwaka huu, baada ya kauli yake ya kupinga mikopo kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na kuzua taharuki hali iliyosababisha baadhi ya watu kushinikiza ajiuzulu nafasi hiyo kwa kile kilichoonekana kupingana na kiongozi wake.

## Mkewe Sabaya: Nitahakikisha mume wangu anakuwa huru

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKE wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ambaye ni shahidi wa pili wa utetezi, Jesca Thomas (28), amedai mahakamani kwamba atafanya kitu chochote isipokuwa kuvunja sheria ili kuhakikisha kuwa mume wake anaachiwa huru.

Kadhalika, alikiri mahakamani kwamba laini za simu alizokuwa akizitumia kufanya mawasiliano hazikusajiliwa kwa jina lake bali mume wake alitumia vitambulisho vyake kusajili.

Shahidi huyo, alitoa madai hayo jana mbele ya hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, katika kesi ya uhujumu uchumi.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Othmed Mtenga, shahidi huyo, alikiri kwamba laini ya simu ambayo alikuwa anaitumia hakusajili kwa jina lake bali kwa jina la Sabaya.

Alidai kwamba kwa kuwa hakuwa na Kitambulisho cha Taifa wala namba, Ole Sabaya alitumia kitambulisho chake kumsajilia laini ya simu.

Aliendelea kudai kuwa Januari 22, mwaka 2021, hakujua kama kuna sehemu Sabaya alikwenda mbali na ofisini kwake.

Kadhalika akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, shahidi huyo aliieleza mahakama hiyo, anatambua haki zake ikiwamo haki ya kumiliki mali na kwa jina lake.

Vile vile, alidai katika mali wanazomiliki zipo ambazo zimeandikwa kwa jina lake ikiwamo gari aina ya VX Masai T342 ANT, na nyingine zimeandikwa kwa majina ya Sabaya.

Alidai laini aliyokuwa anatumia kwa ajili ya kufanya mawasiliano ya kibiashara ilisajiliwa mwaka 2018 kwa ajili ya matumizi binafsi.

Pia alidai kwamba sehemu waliyokamatwa huko Mbezi, mkoani Dar es Salaam ilikuwa ni hotelini na sio 'apartment'.

Alidai kwa mujibu wa mila za Kimasai haruhusiwi kushughulika na suala la mifugo. Kwamba fedha zilizokuwa zinapatikana kutokana na mauzo ya mifugo hiyo walikuwa wanaziweka benki.

"Sabaya alikuwa anafanya biashara ya kuuza mbuzi na ng'ombe, lakini kwa mujibu wa mila zao za Kimasai wanawake hawaruhusiwi kujihusisha na mifugo hivyo akishafanya hela analeta nyumbani bila ya mimi kujua alifanya vipi biashara yake," alidai shahidi huyo.

Kadhalika, alidai wanamiliki mashamba eneo la Malula, Mkoa wa Tanga hekari 11.

Alidai kwamba Juni 4, mwaka 2021, wakati akihojiwa na TAKUKURU na kutoa baadhi ya vitu vya Sabaya, alivitoa kama mke wake na sio mchumba.

Alidai kwamba yupo tayari kufanya chochote ili mume wake awe huru bila ya kuvunja sheria.

Shahidi huyo alidai ndoa yake na Sabaya ilifungwa katika Kanisa la Arusha Central Church mwaka 2018 na Askofu aliyefungisha ndoa hiyo ni Dk. Lekundayo. Kabla ya kufunga ndoa ilitangazwa kwa wiki tatu.

Akijitetea jana, Sabaya alidai kwamba Januari 22, mwaka jana, hakwenda Mkoa wa Arusha wala kufika katika karakana ya mfanyabiashara Francis Mroso, iliyoko Mbauda jijini humo.

Kadhalika alidai kwamba siku hiyo, hakutoka katika kituo chake cha kazi wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alidai kwamba ni mwanasiasa na aliteuliwa Julai 29, 2018 na alidumu kwa nafasi ya ukuu wa wilaya kwa miezi 32.

Alidai kwamba Januari 22 mwaka 2021, majira ya asubuhi alimuaga mke wake, Jesca Thomas, kwamba anakwenda ofisini kutekeleza majukumu yake na siku hiyo alikuwa na kazi ya kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji na alikaa ofisini hadi majira ya saa 11 jioni.

Alidai kazi ya kutatua mgogoro huo, alikuwa akishirikiana na Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, Upendo Uwela.

Shahidi huyo alidai kwamba alifunga ndoa na mke wake, Mei 27, mwaka 2018, katika Kanisa la Wasabato Arusha.

Pia alidai ili gari la serikali litoke nje ya wilaya lazima dereva apewe kibali na Katibu Tawala wa Wilaya kwa kuwa ndiyo mhusika anayetakiwa kuidhinisha na kutoa posho na mafuta ya safari.

Vile vile, alidai utaratibu wa kutoka ndani ya wilaya moja kwenda nyingine, lazima kutoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa kwa kuwa ndiye kiongozi mkuu.

Alidai kwamba kilichozungumzwa mahakamani na aliyekuwa Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Renatus Msangira, kwamba hakupokea taarifa ya Sabaya, dereva na gari kutoka Wilaya ya Hai ni za ukweli kwa kuwa hakuweza kutoa taarifa kwa kiongozi huyo kwa kuwa hakutoka kituo chake cha kazi Januari 22, mwaka 2021.

HABARI KITAIFA

# Sugu apigia debe chanjo corona

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ALIYEKUWA Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi, maarufu kama 'Sugu', amewashauri Watanzania kujitokeza kwenda kupata chanjo ya UVIKO- 19 huku akisisitiza ugonjwa huo una madhara kiafya na kiuchumi.

Akizungumza na Nipashe jana, Sugu alisema ugonjwa wa UVIKO-19 umeathiri mataifa yote duniani, Tanzania ikiwamo hasa kwenye masuala ya kiuchumi, hivyo akashauri ni vizuri hatua zikachukuliwa na Watanzania wakajitokeza kuchanja.

Sugu alisema yeye na familia yake ni miongoni mwa watu walioathirika na ugonjwa huo, biashara zake ziliyumba wakati wa mlipuko na kwamba mmoja wa wanafamilia aliugua na wakatumia gharama kubwa kumtibu.

Mwanasiasa huyo ambaye ni msanii wa mziki wa kufokafoka 'Hip Hop', alisema mmoja wa wanafamilia wake ambaye hakumtaja jina ni miongoni mwa watu waliougua ugonjwa huo.

Alisema kaka yake huyo alianza kujisikia vibaya na alipokwenda hospitalini alipimwa na hakukutwa na ugonjwa wowote lakini baadaye alipelekwa katika Hospitali ya Taifa ya Mhimbili ambako alilazwa kwa muda wa wiki tatu.

Wakati wote huo kaka yake huyo alikuwa amewekewa mtungi wa kumsaidia kupumua na kwamba gharama za matibabu ni kubwa kuliko gharama ya kuchanjwa.

Sugu pia alisema alisema kaka yake huyo aliugua na kutibiwa miezi sita iliyopita lakini mpaka sasa bado hajapona kwa asilimia 100, hivyo akasisitiza kuwa ugonjwa huo una athari kubwa.

"Ukisikia watu wanasema wametumia Sh. milioni 18, 19 mpaka 20 usidhani ni uongo ni taarifa za ukweli kabisa maana mimi nimekutana nazo," alisema Sugu.

Alisema hali ya kaka yake iliwakatisha tamaa wanafamilia wakiamini kwamba asingepona lakini juhudi za madaktari zilisaidia kumwokoa ingawa walitumia gharama kubwa .

Sugu alisema kutokana na madhara yaliyomkuta kaka yake, yeye mwenyewe aliamua kwenda kuchanja, hivyo akafanikiwa kuchanjwa Julai 30, mwaka jana, na akajipiga picha na kuisambaza ili Watanzania wote waone.

Chanjo hiyo, alisema inamsaidia kujikinga na virusi hivyo na kwamba kutokana na faida alizozipata, aliamua kuanza kuwahamasisha Watanzania wengine kuchanjwa.

Pamoja na Watanzania kuendelea kufuata taratibu zote zinazosisitizwa na wataalamu wa afya, alisema wanatakiwa kuendelea kuchanjwa ili kuwa na uhakika wa kutoambukizwa ugonjwa huo.

## Simu za kina Mbowe zapokewa kortini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, imepokea simu nne zikiwamo za Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na mshtakiwa wa kwanza, Halfani Bwire kama kielelezo cha Jamhuri katika kesi ya ugaidi.

Vielelezo hivyo vilitolewa jana na shahidi wa 10, Inspekta Innocent Ndowo, na kupokewa mbele ya Jaji Joachim Tiganga anayesikiliza shauri hilo.

Shahidi huyo akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, alidai ripoti aliyopeleka kwa wapelelezi iliambatana na vielelezo ambazo ni simu nne alizozipa alama ya E,F,G na H.

Alidai akiona anaitambua, miongoni mwa vitu vilivyoko vya kumwezesha kuitambua ni namba ya kesi CD/IR/2027/2020, majina, ina muhuli kwa niaba ya Kamishna wa Uchunguzi wa Kisayansi na ina saini ya Kamishna Msaidizi wa Polisi Naftal Joseph.

Shahidi baada ya kuelezea anavyotambua nyaraka aliomba kutoa kama kielelezo. Upande wa utetezi haukuwa na pingamizi, mahakama ilipokea nyaraka hizo.

Mahakama ilipokea vielelezo hivyo sita, ripoti mbili zilitambulika kielelezo namba 22, 23, simu nne zilitambuliwa kwa IMEI namba 355029115930845 kielelezo namba 24, 353487133305 kielelezo namba 25, 358821101132040 kielelezo namba 26 na 352386071165127 kielelezo namba 27.

Miongoni mwa simu hizo kuna simu ya mshtakiwa Freeman Mbowe, Halfani Bwire na Luteni Dennis Urio ambazo zilifanyiwa uchunguzi wa miamala ya simu na usajili wake.

Shahidi anasoma baadhi ya ujumbe uliokutwa kwenye simu ya Luteni Urio kama ifuatavyo;-

"Tutumie nauli tukutane Morogoro, nipo njiani naelekea Singida, nimepata bro, tutaongea jioni."

"Mh. habari za siku, Salama Kaka, Mhe. mmoja yuko Kigoma mtafanya naye kazi. Unamaliza lini huko? Mwezi wa tatu mwishoni."

"Bro upo. Mara ya mwisho kuwasiliana na wewe ulisema unatoka Mtwara, Ohh kaka nakuombea heri."

Shahidi alimaliza kusoma vielelezo vilivyopokewa mahakamani, upande wa mashtaka walimaliza kumwongoza, zamu ya mawakili wa upande wa utetezi kumuhoji maswali kutokana na ushahidi wake.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanashtakiwa kwa mashtaka sita ikiwamo kulanjama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei na Agosti mwaka 2020.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA WASAFIRISHAJI

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inawakumbusha Wafanyabiashara wote wa usafirishaji kufika kwenye ofisi zetu au kupitia mifumo yetu kwa ajili ya kulipa kodi ya mapato awamu ya kwanza.

*Epuka usumbufu na adhabu kwa kutokuwa na stika ya mapato!.*

Imetolewa na;

MKURUGENZI HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

# Zimamoto: Tulichelewa kupata taarifa za moto Soko la Karume

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala, limesema taarifa za kuungua moto kwa Soko la Karume, Mchikichini zilichelewa kuwafikia.

Kadhalika, limesema linaamini kama taarifa hizo zingefika mapema, wangeokoa mali kwa asilimia kubwa na kuepusha athari kubwa iliyojitokeza katika tukio hilo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mrakibu Msaidizi wa Jeshi hilo Mkoa wa Ilala, Elisa Mugisha, wakati akihojiwa na kipindi cha Super Breakfast cha East Africa Radio, Mikocheni, Dar es Salaam.

Alisema licha ya kufika na kukuta moto umekuwa mkubwa, pia mazingira katika soko hilo hayakuwa rafiki kutokana na kutokuwa na nafasi ya kupitisha gari.

"Watu waliona moto mapema, lakini wakaanza kupambana nao. Sisi tulipata taarifa saa 9:30 usiku, wakati wanatupatia taarifa tayari moto ulikuwa umeshakuwa mkubwa," alisema Mugisha.

"Kulikuwa na magari manne ya kuzima moto na tulizunguka sana kulingana na mazingira ya pale. Taarifa ingetolewa mapema, tungeudhibiti na waliokuwapo walipoona umewashinda wakaanza kuokoa mali zao," aliongeza.

Soko hilo liliungua usiku wa kumkia Januari 16, mwaka huu, huku chanzo chake kikiwa bado hakijajulikana.

Tayari timu ya uchunguzi imeundwa na inasubiriwa ndani ya siku saba kutoa majibu ya chanzo pamoja na athari halisi zilizosababishwa na moto huo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'ilabuzu Ludigija, timu hiyo inajumuisha ofisi yake, ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jeshi la Polisi na la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Pamoja na kuundwa timu ya kufanya kazi hiyo, juzi wafanyabiashara wa soko hilo walifunga barabara na kuandamana hadi ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, wakishinikiza waruhusiwe kujenga vibanda vya muda ili waendelee na biashara. Walidai kuwa hawawezi kusubiri mpaka siku saba kutokana na ugumu wa maisha na sehemu hiyo ndiyo ilikuwa tegemeo lao.

Kutokana na maandamano hayo, Jeshi la Polisi liliwatawanya kwa mabomu ya machozi na baadaye Mkuu wa Wilaya alifika na kuwaomba wavute subira mpaka uchunguzi umalizike.

Mkuu wa Wilaya aliwaruhusu kuweka alama katika maeneo yao na kwamba baada ya timu kumaliza kazi yake kwa muda uliowekwa wataruhusiwa kujenga vibanda vyao.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Ofisa wa Polisi wa Kituo cha Polisi kinachotoa huduma kwa wananchi kupitia njia ya mtandao 'Smart Police Station', Sami Humaid, wakati alipotembelea maonyesho ya Dubai Expo 2020 juzi. **PICHA: IKULU**

# Tanzania kunadi fursa za uwindaji Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajia kunadi fursa za uwekezaji zilizoko katika tasnia ya uwindaji katika Mkutano wa 50 wa Mwaka wa Uwindaji wa Kitalii nchini Marekani, uliondaliwa na Jumuiya ya Uwindaji ya Kimataifa.

Mkutano huo unawakutanisha watunga sera na wafanya uamuzi katika ngazi za juu kutoka nchi mbalimbali duniani. Pamoja na mambo mengine, watajadili masuala ya kisera katika kuendeleza uwindaji.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Maliasili na Utalii ilieleza kuwa Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Damas Ndumbaro, anatarajia kunadi fursa za uwekezaji za uwindaji wa kitalii kwa lengo la kuwawezesha matajiri wakubwa duniani kuchangamkia uwekezaji huo nchini.

"Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amewasili jijini New York, Marekani, anatarajia kunadi fursa za uwekezaji za uwindaji wa kitalii zilizoko nchini kwa lengo la kuwawezesha matajiri wakubwa duniani kuchangamkia uwekezaji huo uliopo hapa nchini," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema Tanzania ni mshiriki muhimu katika mkutano huo kwa sababu ni moja ya nchi zinazoongoza duniani katika uhifadhi wa wanyamapori na uwindaji.

Pia taarifa hiyo ilisema kupitia mkutano huo itaweza kuongeza uelewa zaidi katika masuala ya kisera na uamuzi katika kuendeleza sekta ya uwindaji wa kitalii nchini.

Dk. Ndumbaro, kwa mujibu wa taarifa hiyo, atapata fursa ya kufanya mazungumzo na wadau mbalimbali wa masuala ya utalii ikiwa sehemu ya kuwavutia kuja nchini kuwekeza.

"Katika mkutano huo, Waziri Ndumbaro ameambatana na Mkurugenzi wa Wanyamapori, Dk. Maurus Msuha, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TAWA, Meja Jenerali Hamis Semfuko na Kaimu Kamishna Uhifadhi wa TAWA, Mabula Misungwi.

"Wengine ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa TAWA, Lulu Ng'wanakilala na Ofisa Mhifadhi Mkuu wa Wanyamapori wa kutoka TAWA, Segolin Tarimo." Ilibainisha taarifa hiyo.

Waziri Ndumbaro pamoja na ujumbe wake wamepokewa Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Elsie Kanza.

# 11 kugombea uenyekiti, makamu ACT-Wazalendo

**Na Christina Mwakangale**

JUMLA ya wanachama 11 wa Chama cha ACT-Wazalendo, wametia nia ya kugombea nafasi tatu ikiwamo uenyekiti, makamu mwenyekiti pamoja na ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ndani ya chama hicho.

Wagombea wa nafasi ya Uenyekiti ni wawili akiwamo, Juma Duni Haji pamoja na Hamad Masoud Hamad huku nafasi ya Makamu Mwenyekiti akiwamo Othman Masoud Othman na Juma Said Sanani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na chama hicho na Mwenyekiti Kamati ya Uchaguzi, Joran Bashange, nafasi ya ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa-Tanzania Bara, inawaniwa na wanachama saba akiwamo Chrisant Msipi na Ester Thomas.

Aliwataja wengine ni Fungo Benson, Johnson Gagu, Msafiri Mtemelwa, Jafet Masawe pamoja na Fidel Christopher na kwamba hatua hiyo ya wanachama kutia nia inatokana na Kamati ya Uchaguzi kutangaza kalenda ya kuchukua na kurejesha fomu kuanzia Januari 4 hadi 17, mwaka huu.

"Mnamo Februari 17, mwaka jana, chama chetu kiliondokewa na aliyekuwa Mwenyekiti wake wa Taifa hayati Maalim Seif Sharif Hamad. Kwa mujibu wa ibara za 84(4) na 116(4) za Katiba ya ACT-Wazalendo (Toleo la 2020) nafasi hiyo inapaswa kujazwa ndani ya miezi 12.

"Tayari Halmashauri Kuu ya Taifa kupitia kikao chake cha Oktoba 31, mwaka jana, kwa kuzingatia mamlaka yake chini ya ibara za 69 (2) na 84 (4) za Katiba ya Chama, ilipitisha azimio la kuitishwa Mkutano Mkuu Maalumu wa uchaguzi kujaza nafasi ya Mwenyekiti Taifa, Makamu Mwenyekiti Zanzibar na Mjumbe mmoja wa Halmashauri Kuu ya Taifa kutoka Tanzania Bara na kuteua Kamati Maalumu kusimamia uchaguzi huo," alisema Joram.

Joram alisema baada ya mchakato huo, Kamati ya Uchaguzi itafanya kikao leo, kuandaa taarifa ya uchukuaji na urejeshaji fomu kwa ajili ya kikao cha Sekretarieti ya Kamati Kuu.

Pia, alibainisha kwamba, Sekretarieti ya Kamati Kuu itakaa Januari 22, mwaka huu, ili kupokea taarifa ya watia nia kutoka Kamati ya uchaguzi na kuandaa kikao cha Kamati Kuu ambacho kitaketi Januari 27, mwaka huu, kuandaa mapendekezo ya uteuzi kwa Halmashauri Kuu ya Taifa.

"Halmashauri Kuu ya Taifa itaketi Januari 28, mwaka huu, kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa uenyekiti, Makamu Mwenyekiti na ujumbe wa Halmashauri Kuu Taifa ili kupata majina ya wagombea rasmi na kuwatangaza kupitia mdahalo wa wazi wa wagombea watakaopata fursa kujieleza, kuulizwa maswali," alisema Joram.

Kadhalika, alibainisha Januari 29, mwaka huu, mkutano mkuu maalumu wa uchaguzi utaketi na kupiga kura kuchagua mwenyekiti wa chama, makamu mwenyekiti Zanzibar na mjumbe mmoja wa Halmashauri Kuu ya Taifa."

"Kamati ya uchaguzi inatoa wito kwa viongozi wa chama wote, wajumbe wa mkutano mkuu, watia nia wote na wanachama kwa ujumla, kuhakikisha wote kwa pamoja tunatunza maadili ya chama, kuhakikisha kuwa wanapatikana viongozi tutakaoshirikiana nao kukijenga na kukiimarisha chama kwa mustakabali mwema wa demokrasia nchini," alisema Joram.

HABARI KITAIFA

# Ridhiwani aagiza upimaji utendaji kazi

Na Munir Shemweta

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amewaagiza makamishna wa ardhi wasaidizi wa mikoa kuhakikisha wanawawekea vipimo vya utendaji kazi watumishi wa sekta ya ardhi.

Amesema kila baada ya mwezi mmoja, utendaji wa watumishi hao upimwe lengo likiwa ni kuleta tija kwenye sekta ya ardhi huku akisisitiza wataalamu hao kuwa wabunifu sambamba na kutoa huduma bora na kwa wakati.

Ridhiwani alitoa agizo hilo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi wa mkoa huo na baadhi ya watumishi wa sekta hiyo katika mkoa wa Pwani akiwa kwenye ziara yake baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo hivi karibuni.

"Makamishna wangu, haya sasa ni maagizo. Hao maofisa wenu wote katika idara zenu zote wawekeeni vipimo vya kupima utendaji kila baada ya mwezi mmoja ili kujua nani anafanya kazi na nani hafanyi kazi, kujua idara gani inafanya kazi na idara gani haifanyi kazi" alisema Ridhiwani.

Alisema kama watendaji wa sekta ya ardhi wataendelea kufanya kazi kwa mazoea na kuzalisha migogoro kila siku, sekta ya ardhi haitapiga hatua.



**Kama watendaji wa sekta ya ardhi wataendelea kufanya kazi kwa mazoea na kuzalisha migogoro kila siku, sekta ya ardhi haitapiga hatua.**

Kwa mujibu wa Ridhiwani, baadhi ya watendaji wa sekta ya ardhi nchini ni mafundi wa kuzalisha migogoro na baadaye hupita mlango wa nyuma kujifanya wanakwenda kuimaliza jambo alilolieleza kuwa wizara haiko tayari kuvumilia tabia hiyo kwa kuwa kuna Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS) unaoweza kuzitafutia ufumbuzi baadhi ya kero za ardhi.

"Mfumo wetu wa ILMIS uko vizuri na umeanza mkoa wa Dar es Salaam. Tunataka kuupeleka mikoa mikubwa na baadaye nchi nzima maana tufikie mahali majawabu ya shida zetu tuyapate kupitia mfumo.

Naibu Waziri alisema hatakuwa tayari kusikia Rais Samia Suluhu Hassan anabebeshwa lawama asizostahili kuhusiana na ardhi na kuweka bayana kuwa kama yuko mtu anayedhani anaweza kufanya jambo la ovyo, basi ajue utaratibu huo umekwisha.

Katika hatua nyingine, Ridhiwani aliwataka wataalamu wa sekta ya ardhi kuwa wabunifu sambamba na kutoa huduma bora na kwa wakati na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kuisaidia serikali na wananchi kwa ujumla.

"Nawaomba muwe wabunifu na muache kufanya 'business as usual' (kazi kwa mazoea). Kama kazi yako ni ofisa ardhi usipoletewa vifaa eti unalala, hiyo haiwezekani na kama hakuna vifaa waombe wakubwa wako ili waone sababu ya kupeleka vifaa ili upime ardhi kwa kuwa ardhi ni uchumi," alisema.

# TTB, Azam zakubaliana kutangaza utalii

Na Salome Mwasamale

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) na kampuni ya Azam Media zimetia saini mkataba wa mwaka mmoja wa uanzishwaji wa kipindi cha Shangazwa chenye lengo la kukuza utalii wa ndani.

Makubaliano hayo yamefikiwa baada ya mazungumzo ya muda mrefu yaliyofanywa baina ya taasisi hizo na kila mmoja kujiridhisha kuwa kuna manufaa katika kufanya hivyo.

Akizungumza kabla ya kutia saini mkataba huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TTB, Jaji (mstaafu) Thomas Mihayo (pichani), alisema makubaliano hayo yamefikiwa baada ya mazungumzo ya muda mrefu.



"Mazungumzo yetu ya muda mrefu na Azam yamezaa matunda ndiyo maana leo (jana) tumeamua kutia saini mkataba huu wa makubaliano ya uanzishwaji wa kipindi cha Shangazwa ili kuendelea kukuza utalii wetu wa ndani," alisema.

Kutokana na vyombo vya habari mbalimbali ikiwamo Azam kutangaza kwa bidii kuhusu vivutio vilivyopo nchini, Watanzania sasa wameanza kuwa na mwamko wa kwenda kutembelea vivutio mbalimbali.

Akitolea mfano katika Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwa mwaka 2021 na 2022, Jaji Mihayo alisema Watanzania wengi walijitokeza kwenda kutalii katika hifadhi za Ngorongoro na Serengeti na kusababisha hoteli zote kujaa hali ambayo alisema ilileta taswira nzuri kwa bodi na Watanzania kwa ujumla.

"Kusini kulisahaulika kutokana na miundombinu ya barabara kuwa mibovu lakini sasa serikali imefanya jitihada za makusudi kurekebisha miundombinu ya barabara hali ambayo sasa imetoa fursa ya utalii wa mikoa hiyo kuanza kutangazwa kwa nguvu zote," alisema

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TTB, Felix John na ofisa Masoko Gladstone Mlay, walisema wamejipanga kuhakikisha vivutio vilivyopo mikoa ya kusini vinafufuliwa.

Walitaja baadhi ya vivutio hivyo kuwa ni pamoja na Nyumba Nitu, Bibi Kiyeyeu, Nyerere, Mikumi, Udzungwa na Ruaha.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam Media, Tido Mhando, alisema Shangazwa ni kipindi kipya kitakachoanza kurushwa baada ya kutiwa saini mkataba huo na kitabeba maudhui ya kitalii ikiwamo utamaduni mbalimbali wa kitanzania kama vile makabila, ngoma na viumbe hai.

Alisema kipindi hicho pia hakitaacha kugusa maeneo muhimu kama Mlima Kilimanjaro, Ngorongoro na mbuga za wanyama kwa kuwa ni miongoni mwa vivutio vinavyoitangaza Tanzania barani Afrika na duniani kwa ujumla.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Shule zihimizwe kujikinga na UVIKO -19

**JUMATATU** ya wiki hii shule za msingi na sekondari zilifunguliwa huku asilimia kubwa wanafunzi, walimu na watumishi wengine wakionekana kutochukua tahadhari ya kujikinga na UVIKO-19.

Kwenye shule zilizotembelewa maisha yalionekana kuendelea kama kawaida bila kuchukuliwa tahadhari zozote za kujikinga na UVIKO-19 kwa kufuata mwongozo ulitolewa na Wizara ya Afya.

Baadhi ya shule zilikuwa hazina vyombo vya maji tiririka, sabuni, vitakasa mikono wala uvaaji wa barakoa kwa wanafunzi, walimu, watumishi wengine na wananchi wanaofika maeneo hayo.

Hali hiyo ni tofauti na hamasa inayotolewa kila siku ya kujikinga na UVIKO-19 kutokana na uwezekano mkubwa wa ugonjwa huo kusambaa kwa haraka ikiwa tahadhari haitachukuliwa.

Kwa sasa jitihada zinafanyika kuhakikisha wananchi wengi wanachanja ili kupunguza kasi ya ugonjwa huo watakaoupata, lakini bado watu wengi hawajajitokeza kuchanja.

Madhara ya UVIKO-19 ni makubwa kiuchumi na kiafya, kwa kuwa wapo ambao maisha yao yameharibika kabisa kutokana na ugonjwa huo, kwa kurudi katika hali ya umaskini.

Kwa waliopatwa na ugonjwa huo hata wakipona madhara ya muda mrefu hubaki mwilini na mara kadhaa baadhi ya wagonjwa wamejitokeza kueleza licha ya kupona, bado hawajarudi kwenye afya zao njema.

Zipo taarifa za kisayansi zilizothibitishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), kuwa watoto wanaweza kusambaza ugonjwa huo kirahisi kwa kuwa wanahamisha virusi kutoka eneo moja kwenda lingine.

Hadi sasa hakuna ushahidi wa kisayansi wa watoto kuambukizwa virusi hivyo, lakini upo uwezo wa watoto kuambukiza watu wazima nyumbani na ndiyo maana wanatakiwa kuvaa barakoa, kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono.

Ni muhimu utaratibu wa wanafunzi kunawa mikono mara kwa mara ukarejeshwa kwa kuwa mbali na kusaidia kujikinga na corona inawasaidia kujikinga na maradhi mengine ikiwamo ya homa ya matumbo.

Pia husaidia usafi wa mara kwa mara kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla, hivyo ni muhimu kuhamasisha wanafunzi kunawa na kujikinga na ugonjwa huo ili kuwakinga watu wa nyumbani mwao.


Tunafikiri ni muhimu walimu nao wakawa wanavaa barakoa kama inavyotakiwa ili waendelee kuwa salama, kwa kuwa taarifa za kisayansi zinaonyesha kuwa watu wazima kuanzia miaka 35 kuendelea wako kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa ugonjwa huo kuliko wengine.

Ni muhimu walimu na watumishi wengine wakahakikisha wako salama muda wote, pia wachanje ili watakapopata ugonjwa huo usiwe mkali.

Upo ushahidi wa kisayansi kuwa waliochanja wanaweza kupata corona, lakini ugonjwa hautakuwa mkali kama ambaye hakuchanja na uwezekano wa kupona ni mkubwa.

Lazima kuhakikisha usalama wa kila mmoja wetu katika mazingira yoyote ili kuepuka gharama za matibabu na kuumia kiuchumi kutokana na ugonjwa huo..

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Walimu na wanafunzi UVIKO-19 bado kitisho

Na Jenifer Gilla

**JUMATATU** wiki hii ilikuwa ni siku ya kurudi masomoni kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na walimu wao, baada ya kumaliza likizo ya mwaka wa masomo na mapumziko ya mwaka mpya.

Katika baadhi ya shule za jijini Dar es Salaam, wanafunzi hao wanaporejea shuleni wanapokelewa na walimu wao bila kuchukua tahadhari za ugonjwa corona au UVIKO-19.

Walimu ambao ndiyo walikuwa wapokeaji wa wanafunzi pamoja na wanafunzi wageni hawakuonekana kufuata maagizo yanayotolewa na Wizara ya Afya ya kujikinga na virusi hivyo, ambayo hutangazwa kila mara kwenye vyombo vya habari zikiwamo redio na runinga.

Maagizo hayo ni kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kukaa umbali wa mita moja baina ya watu pamoja na kupata chanjo ya UVIKO-19 ambazo hutolewa kwenye vituo vya afya bure hasa kwa watu wazima.

Katika shule nyingi wanafunzi walionekana kujazana darasani, darasa moja likiwa na wanafunzi 80, wakikaa kwenye madawati ambayo yamekaribiana kiasi cha kwamba hakuna nafasi ya mtu kupita kwa nyuma.

Baadhi ya shule hazikuwa na ndoo za maji za kunawia mikono ambazo zilipaswa kuwekwa kwenye geti la kuingilia na sehemu nyingine ili wageni pamoja na wanafunzi wasafishe mikono yao kabla ya kuingia ndani.

Hata, zile zilizokuwa na ndoo watoto hawakuonekana kuzijali kwani walikwenda kununua vitu na kula bila ya kunawa mikono na hakukuwa na mwalimu wa kusimamia hilo.

Katika shule ya Msingi Ruvuma iliyopo Manispaa ya Temeke, mwalimu wa darasa la kwanza, alikutwa amezungukwa na kundi la wanafunzi wakigombania kusahihishiwa ili wawahi kwenda nyumbani, lakini hakuwa na barakoa.

Katika mazingira hayo, mwalimu huyo ambaye hakuwa na barakoa aliyekuwa akiwatuliza wanafunzi hao waache vurugu, ni rahisi kuambukizana virusi hivyo na wanafunzi hao ambao nao wangekwenda kuambukiza ndugu na jamaa , ambapo ndani ya muda mfupi idadi ya maambukizi na hata vifo ingeongezeka.

Pengine kukaa nyumbani kwa muda mrefu kumewafanya kusahau kuwa ugonjwa huu upo, na hii ni kutokana na kwamba watoto hawakuwa na watu wa kuwakumbusha kuhusu ugonjwa huo hatari kwa kuwa wazazi wanadhani kuwa hilo ni jukumu la walimu.

Kwa kuwakumbusha tu kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), hadi kufikia Januari 3, mwaka huu Tanzania ilikuwa na jumla ya wagonjwa wa UVIKO-19, 30,564 na vifo 740 hali inayoonyesha kuwa maambukizi yanaongezeka ingawa kwa kasi ndogo .

Kama wahenga wanavyosema 'yaliyopita si ndwele', ni wakati uongozi wa shule kutilia mkazo suala la UVIKO-19 kwa kurudisha nidhamu ya woga na hofu juu ya ugonjwa huo kwa watoto.

Walimu hawana budi kuanza upya kuelimisha wanafunzi juu ya ugonjwa huo hatari, jinsi unavyoambukiza na athari zake kwa afya zao, lakini pia njia muhimu za kujikinga na ugonjwa hupo.

Kwa kuwa kujifunza kwa kuona na vitendo ni bora zaidi walimu wanapaswa kuonyesha mfano kwa kuvaa barakoa kila wakati, kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono wakiwa darasani ili wanafunzi wajifunze kutoka kwao.

Umma unapaswa kuunga mkono juhudi za serikali kwa kazi kubwa inayofanywa ya kuhakikisha kuwa Watanzania wanaishinda vita dhidi ya UVIKO-19, kwani kasi ya maambukizi nchini sio kubwa ikilinganishwa na nchi nyingine kama vile Russia ambayo mpaka kufikia January 16 ilikuwa na jumla ya wagonjwa milioni 10.8 wagonjwa wapya wakiwa 31,252 na vifo vipya 688 kwa mujibu wa mtandao wa World meter.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Naliendele, Fortunas Kapinga (kushoto), akiwaonyesha wanafunzi kutoka Chuo cha Taifa cha Ulinzi, baadhi ya juisi zilizotengenezwa kwa zao la korosho, walipotembelea kituo hicho, mkoani Mtwara jana. **PICHA: ABDALLAH KHAMIS**

# Nape aagiza kukamilika anwani makazi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amefungua mafunzo ya kujenga uelewa wa anuani za makazi kwa viongozi wa mkoa wa Pwani, huku akitoa agizo kwa mkoa kutekeleza mradi huo kwa muda uliopangwa.

Alisema ifikapo mwezi Mei, mwaka huu, wizara yake inatarajia kumkabidhi Rais Samia Suluhu Hassan, taarifa kamili ya kukamilika kwa anwani za makazi.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya kujenga uelewa wa anwani hizo kwa viongozi na wataalamu, yaliyofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, mjini Kibaha.

Alisema serikali imeamua kutekeleza mradi huo kurahisisha mawasiliano kwa wananchi wake, lengo ni kuhakikisha kunakuwa na anwani za makazi na wizara yake itasimamia ipasavyo ili ukamilike kwa wakati.

Alisema mradi huo ulitakiwa kufanyika kwa miaka mitano, lakini kwa sasa utatakiwa kukamilika Mei 22, mwaka huu, baada ya kuonekana ni muhimu kusaidia sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika mwezi Agosti.

Kwa mujibu wa Waziri Nape, Pwani ni kati ya mikoa ambayo viongozi wake tayari wamepatiwa mafunzo, lakini hadi sasa utekelezaji wake ni asilimia moja na ni kata tatu pekee kati ya 139 ambazo zimeanza kutekeleza mradi huo.

"Tumekuja kukaa na Mkuu wa mkoa ili waone namna ya kufanya, kujipanga na kutekeleza mradi huu kwa muda, hakuna kuongeza muda na ninasema hatutashindwa, wizara yangu itakabidhi mradi kwa wakati," alisema.

Alisema mradi huo unahusisha uwekaji wa nguzo na vibao kwenye mitaa na kwa mkoa huo nguzo 75,392 na vibao 912,640 zinahitajika kufanikisha mradi huo.

Alimtaka Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, kuweka mipango ya kutekeleza mradi huo na wakuu wake wa wilaya na wizara iko tayari kutoa ushirikiano.

"Kikubwa ni mipango mizuri ya kuweza kulitekeleza hili kwa kushirikiana na wakuu wa wilaya, sisi kule wizarani tumeweka utaratibu wa kupata taarifa kila baada ya wiki mbili tujipange kuanzia vijijini na kwenye mitaa," alisema.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ajira na kusaidia kuimarisha ulinzi na usalama kwenye maeneo husika.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Clarence Ichwekeleza, alisema anwani za makazi zinarahisisha kufika kwenye maeneo kwa urahisi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Pwani, alisema suala la anwani litarahisisha kuelewa kila mmoja anakaa wapi.

Vile vile, Kunenge alisema kufanyika kwa mradi huo, mkoa utakuwa na manufaa hususani upande wa viwanda na wanaohitaji kufika kupata bidhaa watapata urahisi.

"Anwani za makazi zikikamilika itarahisisha kama mtu anataka kufika kiwanda fulani inakuwa rahisi kwake kwenda kufuata bidhaa anayoitaka, mimi ninaahidi ushirikiano kwa wizara kufanikisha hili," alisema Kunenge.

# Stanbic Bank yaidai kampuni bil.5/- za mkopo

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya kifedha ya Stanbic Bank (T) Limited imeipeleka mahakamani kampuni inayojishughulisha na usafirishaji, Nam Enterprises Limited kwa madai ya kutolipa mkopo wa zaidi ya Shilingi bilioni tano.

Benki hiyo inaishtaki kampuni hiyo na wakurugenzi wake wanne baada ya kushindwa kulipa mkopo wa Dola za Marekani 2,479, 005.58.

Shauri hilo limeshasikilizwa na Jaji Haruna Songoro wa Mahakama Kuu, Kitengo cha Biashara, ambaye ameamuru kampuni hiyo na wakurugenzi waliodhamini mkopo huo kulipa fedha hizo.

Katika shauri hilo Jaji aligundua kuwa benki imethibitisha madai husika na kwamba kulikuwa na mkopo ambao haujalipwa na kuwataka wadaiwa hao kurudisha fedha hizo na kuwaamuru kulipa gharama za kuendesha shauri hilo.

Hata hivyo, kampuni na wakurugenzi hao walikimbilia Mahakama ya Rufani ambako waliwasilisha taarifa ya kukata rufaa na kufanikiwa kuomba kusimamisha utekelezaji wa hukumu hiyo.

Gavana wa Benki Kuu, Profesa Florens Luoga, hivi karibuni alitoa waraka akieleza kuwa baadhi ya benki na taasisi za fedha zimekuwa zikitoa mikopo bila kufuata taratibu na kusababisha mikopo isiyolipika (NPLs) katika sekta ya benki.

Alitaja tabia hiyo kuwa husababishwa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu wanaoshirikiana na wakopaji. Benki Kuu ilieleza kuwa itawafungia watumishi waliohusika na kuwazuia kuajiriwa katika benki au taasisi yoyote ya fedha nchini Tanzania.

Kwa benki ambazo wafanyakazi wake wana NPLs na benki nyingine, Gavana wa Benki Kuu aliagiza taarifa zao ziwasilishwe Ofisi ya Marejeleo ya Mikopo kwa hatua stahiki.

Benki Kuu pia ilizitaka benki na taasisi za fedha kutotoa mikopo kwa wakopaji wasio waaminifu waliokopa kwa nia ya kutorejesha mikopo hiyo, au wanaotumia udanganyifu kukopa.

Alisema taarifa za wakopaji zinapaswa kuwekwa kwenye daftari maalumu ambalo litashirikishwa na benki na taasisi nyingine za fedha.

Wakati huo huo, kampuni inayodaiwa imepewa miezi mitatu ya kurejesha mkopo huo kabla ya maelezo yao kuingizwa kwenye daftari maalumu.

Benki Kuu ilifanya mapitio ili kubaini sababu kuu za mikopo chechefu katika sekta ya benki na kubaini kuwa watumishi wa baadhi ya benki na taasisi za fedha wanawajibika moja kwa moja kupitia utoaji wa mikopo bila kufuata taratibu ambayo ni sawa na kukosa uadilifu.

Kiwango cha juu cha mikopo chechefu ni miongoni mwa sababu kuu za viwango vya juu vya mikopo na inaweza kusababisha kuyumba kwa sekta ya benki.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HEALTH, COMMUNITY DEVELOPMENT, GENDER, ELDERLY AND CHILDREN

TMDA

TANZANIA MEDICINES AND MEDICAL DEVICES AUTHORITY
ISO 9001: 2015 CERTIFIED

PUBLIC ANNOUNCEMENT (RE-ADVERTISED)

10th November 2021

PAYMENT OF ANNUAL RETENTION FEES FOR THE YEAR 2022

1. The Tanzania Medicines and Medical Devices Authority wishes to remind its esteemed Customers that as per Section 55 (b) of the Tanzania Medicines and Medical Devices Act, Cap 219, the retention of products in the Register of Registered Products is upon payment of a prescribed fee.
2. The Retention Fee is required to be paid by 31st of January of each calendar year as prescribed in the TMDA Fees and Charges Regulations, 2015 and its amendment Regulations of 2017.
3. Please be informed that in – line with the Regulations highlighted above, after 31st January 2022, **Import Permits** will not be issued to any product for which its Annual Retention Fee is not paid.
4. All companies are required to collect the respective invoices from TMDA Sub-Head Offices (located at Off Nelson Mandela Road, Mabibo External, P.O. Box 77150, **Dar es Salaam**) and pay the annual retention fees for the calendar year, 2022 before the 31st January 2022.

**Issued by: The Director General**
**Tanzania Medicines and Medical Devices Authority,**
**P.O. Box 1253, Dodoma.**
**Tel; +255 222 450512/658 445222/777 700002**
**Fax; +255 222450793**
**Email: info@tmda.go.tz**



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Msinune, Wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, wakiwa na mabegi ya kubebea vitabu na madaftari waliyopewa msaada na Taasisi ya Flaviana Matata, wilayani humo, jana. Jumla ya wanafunzi 390 walinufaika na msaada huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo wa GIMIS sasa kuboresha utendaji kazi

**Na Elizabeth Zaya**

KAMISHNA wa Sera za Ununuzi wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Fredrick Mwakibinga, amesema mifumo ya kielekroniki ya Integrated Management Information System (GIMIS), kwa Mawakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini ni muhimu kwenye kuboresha utendaji kazi.

Dk. Mwakibinga alitoa kauli hiyo wakati wa mafunzo kwa watumishi wa taasisi za ununuzi yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Alisema uwapo wa mifumo hiyo ni agizo la serikali na imedhamiria kuongeza tija kwa huduma ili ziwafikie kwa haraka na ubora.

Alisema miongoni mwa faida zinazopatikana kutokana na uwapo wa mifumo hiyo ni pamoja na kupunguza matumizi makubwa ya karatasi, kuokoa muda na pesa.

"Pamoja na changamoto chache zilizopo kama vile utayari wa wadau, faida zake ni kubwa na muhimu zaidi, kwa hiyo ni vyema tukahakikisha tunautumia," alisema Dk. Mwakibinga.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa mfumo huo wa GPSA, Prof. Geraldine Rasheli, alisema mfumo huo utasaidia kuleta mapinduzi katika utoaji wa huduma za Wakala ikiwamo ununuzi wa pamoja wa magari ya serikali, huduma ya ugomboaji, vifaa pamoja na mafuta.

"Kupitia mfumo huu wa GIMIS, wateja wataweza kutuma nyaraka mbalimbali na kufuatilia zilipo, kuona vifaa vilivyoko na bei zake pamoja na bakaa ya amana watakazoweka katika sehemu yoyote wanapokuwapo ambako kuna intaneti," alisema Prof. Rasheli. Na mfumo huu wa GIMIS umeandaliwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA)."

# Atishia kumsweka ndani mkandarasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, ametishia kumsweka ndani mkandarasi ambaye anatekeleza mradi wa barabara kwa kiwango cha changarawe kutoka Kahama hadi Bulyanhuru kilomita 70, baada ya kutoridhika na utekelezaji wake.

Kiswaga alibainisha hayo jana kwenye kikao cha Bodi ya barabara mkoani humo, kuwa baadhi ya wakandarasi wanapewa kazi za kutekeleza miradi ya barabara lakini hawana sifa.

Alisema barabara hiyo ya kutoka Kahama hadi Bulyanhuru ni mbovu na wanapata shida kwenda maeneo hayo kutekeleza shughuli za serikali na kuwahudumia wananchi, utekelezaji wake upo chini ya kiwango na hauna kasi.

"Mheshimiwa Mwenyekiti katika utekelezaji wa miradi hii ya barabara kuna mkandarasi ambaye anatekeleza barabara hii ya kutoka Kahama kwenda Kakola Bulyanhuru kilomita 70, nadhani hana uwezo na ipo siku nitamsweka ndani," alisema Kiswaga.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala Frola Sagasaga, alisema barabara hiyo ni mbovu, na wamekuwa wakitukanwa na wananchi kuwa wameshindwa kusimamia, imekuwa kikwazo kikubwa katika shughuli za kiuchumi na hata utekelezaji wake upo chini ya kiwango.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema hivi karibuni alipita kwenye barabara hiyo na kupata shida kutokana na ubovu na kuagiza kama mkandarasi huyo hana sifa aondolewe kwa kufuata taratibu na kupewa ambaye ana sifa.

Katika hatua nyingine, aliwataka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), (TARURA) na Wakurugenzi, kusimamia sheria za utunzaji wa miundombinu ya barabara, kwa kuzuia magari yenye uzito mkubwa kupita kwenye barabara zinazokataza magari hayo, pamoja na kudhibiti shughuli za binadamu kando kando ya barabara hizo.

Pia, aliwaonya wananchi wa mkoa huo kuacha tabia ya kutupa taka kwenye mitaro ya maji, hali ambayo inasababisha mifereji kutopitisha maji na kuharibu mitaro hiyo, ikiwamo na miundombinu na kuingiza gharama serikali ya kutenga fedha kila mwaka za matengenezo.

Kaimu Meneja TANROADS, mkoani Shinyanga Mhandisi Ferdinand Mdoe, alitoa ufafanuzi ujenzi wa barabara hiyo kuwa kuna wakandarasi watatu, lakini mmoja amepata changamoto na kuahidi kulifanyia kazi ili barabara hiyo itekelezeke haraka na kwa ubora.

Alitaja bajeti ya matengenezo ya barabara katika mwaka wa fedha (2021-2022) kuwa waliomba Sh. bilioni 13.7, lakini wakapewa bilioni 12.2 ambazo ndizo zinatekeleza barabara hizo na kubainisha katika mwaka wa fedha (2022-2023) wameomba tena kiasi kama hicho cha fedha Sh.bilioni 13.7, pamoja na fedha za maendeleo ya barabara Sh. bilioni 2.7..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISI WA UMMA

PONGEZI



**Dr. Laurean Ndumbaro**
*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora*



*Mhe. Jenister Joakim Mhagama*
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora*



*Mhe.Deogratius Ndejembi, Naibu Waziri Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora*



*Bw. Xavier M. Daudi*
*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawa Bora*

Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inampongeza Mhe.Jenister Joakim Mhagama kwa kuteuliwa na Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na inampongeza pia Bw. Xavier M.Daudi kwa kuteuliwa na Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
Pia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inampongeza Mhe.Deogratius Ndejembi Naibu Waziri Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Dkt.Laurean Ndumbaro Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuaminiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kuendelea na nyadhifa zao katika Wizara ya Utumishi.

Sekretarieti_ya_Ajira Sekretarieti ya Ajira Sekretarieti ya Ajira @ajirapsrs

## SHIVYAWATA yaomba kupewa elimu ya chanjo UVIKO-19

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHIRIKISHO la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuwapatia elimu ya UVIKO-19 na chanjo ili kuwakinga na janga hilo ambalo limeibuka kwa awamu ya nne na kutishia maisha.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Charles Kafuku, wakati akizungumza na gazeti hili watu wenye ulemavu walivyofikiwa na kupatiwa elimu ya UVIKO na chanjo yake.

Alisema kundi hilo limesahaulika kupatiwa elimu ikilinganishwa na makundi mengine. Alisema, kundi hilo lina hofu ya chanjo hiyo na wanaamini wakichoma wanaweza kupata shida hapo baadaye na kwamba elimu ingewafikia kwa wakati wangeondoa hofu hiyo na kujitokeza kupata chanjo hiyo.

"Mimi nilipata chanjo kwa mara ya kwanza Desemba 20, mwaka jana, katika zahanati ya Igunga mkoani Tabora na dozi ya pili na mwisho nitachoma mwezi huu tarehe 20, nilipopata chanjo kwa mara ya kwanza nilikwenda kuwaeleza wenzangu, lakini mwitikio ulikuwa mdogo," alisema Kafuku. Alisema, mwitikio wa watu wenye ulemavu kujitokeza kupata chanjo uko chini ikilinganishwa na makundi mengine yakiwamo ya wazee na ili kuondoa changamoto hiyo wahusika wanatakiwa kuwafuata kwenye vijiji, mitaa na kata kuwapatia elimu na kuwaondolea hofu waliyonayo.

Kwa upande wa mratibu wa chanjo, Mukola Vedastus, alisema, mwitikio wa wananchi kujitokeza kupata chanjo ni mdogo tofauti na awali ilivyokuwa na asilimia kubwa wanaojitokeza ni wanaokwenda kumalizia dozi ya pili baada ya kupata ya kwanza.

Hata hivyo alisema, ili wananchi na makundi maalumu yaweze kuchanja, analazimika kuwafuata kwenye maeneo yao na kuwapatia elimu ya muhimu wa chanjo hiyo na kukubali kuchanja.

Pia aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa huo kwa kunawa mikono na maji tiririka, kuvaa barakoa wakati wote, kutakasa mikono na kuepuka kwenda kwenye mikusanyiko isiyo ya lazima ili kujikinga na janga hilo.

# Hati za kimila 4,000 zatolewa Mbarali

**Na Friday Simbaya,** MBARALI

WANANCHI wa vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya wamepimiwa ardhi na kupatiwa hati za hakimiliki za kimila (CCROs), huku baadhi yao wakisema hatua hiyo inawafungulia milango ya kujikomboa kiuchumi, kwa kuwa hati hizo zitawawezesha kukopesheka na taasisi za kifedha.

Hati hizo zimetolewa chini ya mradi wa urasimishaji ardhi unaotekelezwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Land Tenure Assistance (LTA), hatimiliki za kimila zaidi ya 4,000 zimetolewa kwa vijiji vitatu vya Itamba, Ilongo na Ukwama katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya.

Mustapha Issa, Mkurugenzi wa Shirika la Urasimishaji Ardhi Tanzania (LTA), alisema lengo kuu la mradi ni kusaidia wananchi kupima ardhi yao na kuhakikisha kwamba wanapata hatimiliki za kimila kwa kila kipande ambacho kimepimwa.

Aliongeza kuwa lengo kuu lilikuwa kuondoa migogoro ambayo mara nyingi inasababisha kudumaza shughuli za ardhi.

Issa alisema kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na halmashauri ambazo mradi unafanya nao kazi, Iringa, Mbarali, Mbeya na Kilolo, wanaandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuwapimia wananchi na kupewa hati za umiliki wa kimila (CCROs).

"Changamoto kubwa ambazo tumekutana nazo katika utekelezaji wa mradi hasa kwa awamu ya pili ilikuwa ni uchangiaji. Maana yake awamu ya pili lengo lilikuwa ni kuhakikisha hata baada ya ufadhili wa USAID kukamilika wanaendelea na zoezi hilo la urasimishaji ardhi," alifafanua Issa.

Issa aliongeza kuwa vijiji hivyo vitatu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wametoa hati miliki za kimila zaidi ya 4,000 kwa ambao wamechangia, lengo lilikuwa kutoa hati 6,000 na zoezi linaendelea.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, kuna jumla ya vijiji 102 na mpaka sasa wameweza kutambulisha mradi kwenye vijiji 11 na kati ya hivyo, wamekamilisha vijiji vitatu.

Chezalina Mbinga mkazi wa Kijiji cha Itamba, Kata ya Mapogolo, alisema hati hiyo itamsaidia kupata mkopo benki na pia kupungua kwa mgogoro na jirani yake.

Ritta Kanjeli ambaye ni mjane, mkazi wa kijiji cha Ilongo, alisema kuwa na hati hiyo kimemtoa kizani na kuipongeza serikali kutambua umuhimu wa wanawake kumiliki ardhi binafsi.

Eda Mwakapinya pia mkazi wa kijiji hicho alisema kuwa hati hiyo inaenda kupunguza ugomvi wa viwanja kwa kuwa hapo mwanzo kulikuwa na migogoro ya ardhi.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbarali, Michael Semindu, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbarali Reuben Mfune, aliwataka wananchi waliopata hati hizo kuzitunza kama mboni ya jicho kwa kuwa ni mali.

Alisema kuwa hati hizo wanaweza kuchukulia mikopo katika taasisi mbalimbali ya fedha na zimeongeza thamani ya ardhi yao.



Mbunge wa Kalenga, mkoani Iringa, Jackson Kiswaga (kulia), akiteta jambo na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Salim Abri, wakati wa kikao cha kupitia taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya 2020 /2025 kwa kipindi cha mwaka moja uliopita, mjini Iringa jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# DC ataka utaratibu kulipwa walengwa TASAF kuboreshwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amebainisha changamoto wanazozipata walengwa wa TASAF kufuata pesa benki na kukaa foleni muda mrefu na wengine kutoka mbali.

Mboneko alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema na walengwa wa TASAF, Manispaa ya Shinyanga, uliofanyika Mtaa wa Mapinduzi Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga.

Alisema suala la malipo ya pesa benki kwa walengwa wa TASAF linapaswa kuboreshwa, kutokana na wazee hao kukaa benki muda mrefu na wengine kutoka mbali, hali inayohatarisha afya zao na usalama na kusababisha mmoja wa walengwa hao kufariki dunia.

"Hivi karibuni nilipita benki ya NMB nikakuta foleni ndefu sana ya wazee ambao ni walengwa wa TASAF wakisubiri kupata pesa zao jambo ambalo sikufurahishwa nalo sababu wazee wetu wanateseka sana na wengine kutoka mbali, ambapo majuzi tu mama mmoja alifariki dunia akifuata pesa hizo benki," alisema Mboneko.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya aliwataka walengwa wa TASAF kuendelea kuwa wavumilivu katika suala hilo la malipo ya pesa kupitia benki, wakati serikali ikiendelea kuwaboreshea huduma hizo za malipo wasipate usumbufu.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema changamoto zote za walengwa wa TASAF zinafanyiwa kazi, na ameshatoa agizo kwa waratibu wa TASAF kuzishughulikia, pamoja na wale ambao video vyao havisomi kwenye mfumo walipwe kwa njia ya kawaida.

Alitoa wito kwa walengwa wote wa TASAF mkoani humo, wazitumie fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa na wawekeze kwenye miradi yenye tija ambayo ndiyo itawatoa kwenye umaskini.

Naye Mratibu wa TASAF Manispaa ya Shinyanga, Octavina Kiwone, alisema changamoto hiyo ya malipo kwa mfumo wa benki, pamoja na makato ya fedha za walengwa, tayari ameshazungumza na meneja wa benki husika na linafanyiwa kazi.

Aidha, alitaja idadi ya walengwa ambao wapo kwenye mpango wa TASAF 111 awamu ya pili, kuwa ni 800 kati ya 1,215 na kaya hizo zilipita kwenye mchujo, 415 zilikosa sifa na kuondolewa na kubainisha kuwa katika awamu hiyo pia wamepata Sh. bilioni 1.1 ambazo watawapatia walengwa.

Awali, baadhi ya walengwa hao wa TASAF, kwa nyakati tofauti walisema wamekuwa wakipata shida kulipwa pesa zao kupitia benki, kwa kukaa muda mrefu pamoja na pesa hizo kukatwa makato ya benki na kuzitumia pia katika nauli na kusababisha kupata fedha pungufu ambazo wanashindwa kuzitumia vizuri ili kuwatoa kwenye umaskini.

Pia baadhi ya walengwa walitaja mafanikio ambayo wameyapata kupitia fedha hizo akiwamo Christina Ndimila, ambaye awali alikuwa akiishi kwenye nyumba ya tope, baada ya kuingia kwenye mpango huo anaishi kwenye nyumba imara ya bati.

Naye Farida Wiliam, alisema baada ya kuanza kupata fedha za TASAF, alianza kununua bata wa kufuga na kuwa wengi ambao aliuza na baadhi fedha ana nunua mabati, na sasa ameshafikisha bati 20 ambazo anatarajia kuezeka kwenye nyumba yake.

HABARI KITAIFA

# Watumia maji ya mto baada mradi kutokamilika

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WANANCHI wa Kijiji cha Mkwanga, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, wapo hatarini kiafya kutokana na kulazimika kutumia maji yasiyo salama ya Mto Kaseke baada ya mkandarasi anayesimamia mradi wa maji katika kijiji hicho, Howard Consulting Company na anayetekeleza Serengeti Company Limited, kushindwa kukamilisha mradi huo tangu Mei, mwaka jana.

Mkazi wa kijiji hicho, Amina Bahita, alisema maji wanayotumia yamechanganyika na taka nyingi zinazokokotwa na kusafirishwa kwenye mto huo kutoka maeneo mbalimbali na mifugo ikichangia maji hayo.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkwanga, Paulo Ntibalio, alisema suala la maji katika kijiji cha Mkwanga ni kero ya muda mrefu inayohitaji ufumbuzi wa haraka ili kunusuru afya za wananchi wa eneo hilo ambao wanalazimika kutumia maji yasiyo salama kwa kipindi kirefu.

"Hayo maji ya Mto Kaseke hata ukiyatazama tu kwa macho huwezi kutamani kuyaweka mdomoni," alisema.

Akizungumzia suala hilo Meneja Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), Respicious Mombeki, amesema wanahisi kasi ya mkandarasi ni ndogo au kuzidiwa na miradi mingi na wanapambana ikiwezekana anyang'wanywe mradi huo ili wapewe wao waumalizie.

Alisema wanajitahidi kufuatilia ili wananchi wapate maji kwa wakati ingawa wanashindwa kutoa uamuzi wa moja kwa moja kwa mkandarasi kwa kuwa ni mkataba wa utekelezaji wa mradi huo ulifanyika kati ya mkandarasi na Shirika la ENABEL ambao ndiyo wadhamini wa mradi huo.

"Walipaswa wamalize tangu Mei 31, akaongezewa hadi Oktoba 31 na baadaye Desemba 31, lakini bado ameshindwa kukamilisha," alisema.

Mkandarasi alipotafutwa kueleza sababu za kutokukamilisha mradi huo, hakuwa tayari kutoa majibu yoyote.



Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Hamad Kombo (kushoto), akizungumza katika mkutano wa wadau wa kupinga vitendo vya udhalilishaji, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, eneo la Tunguu, kisiwani humo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## ACT-Wazalendo Ruvuma yashauri ruzuku ya pembejeo

**Na Amon Mtega,** SONGEA

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo mkoani Ruvuma, Mshamu Ngabuja, ameishauri serikali iangalie namna bora ya kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo (mbolea) ili kuwasaidia wakulima kununua kwa bei ya chini.

Akizungumza jana na vyombo habari mkoani humo, alisema kumekuwapo na mfumuko wa bei ya vitu ikiwamo pembejeo jambo linalowafanya baadhi ya wakulima hasa wa mikoa ya kilimo kama Mkoa wa Ruvuma kushindwa kumudu bei hizo.

Ngabuja alisema, serikali ikiweka ruzuku kwenye pembejeo hizo itawasaidia wakulima kununua bei ya chini tofauti na sasa mfuko mmoja wa mbolea wa kilo 50 huuzwa kuanzia Sh. 85,000 kulingana na aina ya mbolea.

Alisema licha ya kuwapo kwa changamoto za hali ya hewa katika msimu wa mwaka huu, wakulima wengi hasa wa Mkoa wa Ruvuma wamelima mashamba yao kwa mvua inayoendelea kunyesha huku changamoto kubwa ikiwa ni pembejeo kuwa bei kubwa.

Kwa upande wake, Katibu wa ACT-Wazalendo, Mkoa wa Ruvuma, Richard Tawe, alisema kuwa ili mkulima aweze kujikwamua kupitia kilimo ni lazima kumsaidia kwenye suala la pembejeo ili chakula kiweze kupatikana kwa wingi.

Akizungumzia chama chao, alisema mpango kazi wake ni kujipanga kwenda kwenye mkutano mkuu kumpata mwenyekiti wa chama hicho ngazi ya taifa.

**Alisema licha ya kuwapo kwa changamoto za hali ya hewa katika msimu wa mwaka huu, wakulima wengi hasa wa Mkoa wa Ruvuma wamelima mashamba yao kwa mvua inayoendelea kunyesha huku changamoto kubwa ikiwa ni pembejeo kuwa bei kubwa.**

# Taasisi yahamasisha wananchi chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya na kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19, kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo unaoendelea kuangamiza watu duniani.

Aidha, wamekumbushwa kuwa hawaishi kisiwani na kwamba, kutochukua tahadhari zinazoelekezwa na wataalamu wa afya ni sawa na kuweka rehani maisha yao.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania CEGODETA, Thomas Ngawaiya, alipokuwa akizungumza na gazeti hili kuhusu msimamo wa taasisi kuhusu chanjo ya UVIKO.

"CEGODETA hatuwezi kwenda kinyume na maelekezo ya serikali kuhusu corona na tunatambua kuwa Tanzania sio kisiwa ambacho hakififikiwi na watu wengine, hivyo suala la chanjo ni muhimu," alisema Ngawaiya.

Alisema, dunia kwa sasa ni kijiji na kufafanua kuwa kuna mwingiliano mkubwa wa watu kutoka mataifa mbalimbali na kwamba bila kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa ni sawa na kujiweka hatarini.

"Wizara ya Afya inasema, kufikia Desemba 18, ni watu milioni 1.27 walikuwa wameshapata chanjo kamili ya kujikinga na ugonjwa huo. Kwa takwimu hizi ni wazi kwamba kuna haja Watanzania kuhamasika kupata chanjo," alisema.

Alisema, wizara hiyo inaweka wazi kuwa idadi ya sampuli nyingi zinazopokewa katika Maabara Kuu ya Taifa, zimekuwa zikiongezeka kutoka 14 kwa siku hadi kufikia 47, hali inayoashiria kuwa ni ongezeko la maambukizi.

"Kwa hali kama hiyo, CEGODETA tumeona kuna haja ya kuwakumbusha kwamba wajitokeze kuchanja, lakini wazingatie maelekezo yanayowataka kwa lengo la kuwa salama wawapo katika shughuli za kila siku," alisema.

Kadhalika, alisema mwongozo wa udhibiti wa ugonjwa huo kupitia afua ya kudhibiti misongamano katika jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi, toleo la kwanza la Julai mwaka jana, umeainisha mambo mengi.

Alisema, mwongozo huo umeainisha maeneo mahususi yanayohitaji kutiliwa mkazo kupitia afua za kupunguza msongamano katika jamii ili kukata mnyororo wa maambukizi ya UVIKO-19 kuanzia ngazi ya kaya hadi jamii.

"Unaelekeza kusitisha mikusanyiko mikubwa isiyokuwa ya lazima, ikiwamo ya kijamii, kidini, kisiasa na kama kuna ulazima wa mikusanyiko, kibali kiombwe kuanzia ofisi za serikali za mitaa," alisema.

Alitaja maeneo mengine yanayoguswa na mwongozo huo kuwa ni vyombo vya usafiri na stendi za mabasi, daladala na bodaboda, ambako ugonjwa huo unaweza kusambazwa kupitia vyombo hivyo.

"Iwe mitaani, vyombo vya usafiri, watu wamejisahau na pia hawajitokezi kwa wingi kuchanjwa. Ikumbukwe kampeni ya chanjo ilizinduliwa na Rais Samia Julai mwaka jana, lakini tunaona idadi ya waliojitokeza kuchwanja ni ndogo, ndiyo tukaona nasi tuwahimize wakachanje," alisema.

Salamu kwako spika ujaye...


Ukurasa 12

Ukurasa 14



**MWANADIPLOMASIA ABDALLA HAMDOK Alivyowaangusha Wasudani, wakosa imani naye, ang'oka**

siasa

JUMATANO JANUARI 19, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Wingi makada CCM kuwania uspika unapohusishwa na kuchangamkia fursa

## •Idadi ndogo ya wanawake yatetewa

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA hujengewa fikra na imani kuwa ili 'utoke kimaisha' ni lazima kupitia barabara ya siasa, kunatajwa kuwa chanzo cha msukumo mkubwa na ari ya wana CCM 70 kuchukua fomu ya kuziba nafasi ya uspika, iliyoachwa wazi na Job Ndugai, aliyejiuzulu hivi karibuni, kutokana na kauli yake kuhusu mikopo mipya na kuongezeka kwa deni la taifa.

Kwa sasa fomu za wagombea 70 zimeshapokelewa na mchakato unaendelea ndani ya chama hicho ukiwa ni wa kuchuja waliojitokeza, ili hatimaye wapatikane wale ambao watachuana katika kinyang'anyiro kwa ajili ya kumpata atakayeziba nafasi hiyo kwa kupigiwa kura bungeni mwanzoni mwa mwezi ujao.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wakizungumzia kwa nini watu wengi wamejitokeza kiasi hicho kuwania nafasi hiyo,akiwamo Godwin Gonde ambaye ni Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam, anasema, Watanzania wamejengewa mfumo ambao wanaamini kuwa njia pekee ya kutoka na kufanikiwa kimaisha ni kupitia siasa.

"Wanaamini kuwa kila mmoja ana haki kuwaania nafasi yoyote ndani ya chama na hata serikalini, na wanachukulia kama jukwaa la kutaka kujulikana ili kupimwa na hatimaye kuchaguliwa," anasema Gonde.

Anasema, mazingira hayo ndiyo yanawafanya wajitokeze kwa wingi, na hata wakati mwingine bila kujipima kama wana uwezo wa kuongoza mhimili huo na kwamba wanaangalia kile wanachotarajia kukipata baada ya kuchaguliwa.

"Wengine wanaangalia uchaguzi wa ndani ya chama utakaofanyika mwaka huu, wanataka kujitangaza kupitia njia hiyo ya kuwania uspika ili iwe rahisi kujulikana kwa wana CCM na Watanzania kwa ujumla," anasema.



Stella Manyanya.



Sofia Simba

**KUCHANGAMKIA FURSA**

Mjumbe wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda, anasema, siku hizi wanasiasa wamekuwa ni wepesi wa kuchangamkia fursa kwa lengo la kujinufaisha wao na familia zao kiuchumi na kimapato.

"Ni haki yao kuwania nafasi hiyo, lakini binafsi ninaamini kuwa kinachosumbua wengi ni fursa kwa ajili ya kupata maslahi manono zikiwamo fedha na heshima kwenye jamii pamoja na familia zao, lakini pia wanataka wawe kwenye rekodi," anasema Mwakagenda.

Kuhusu rekodi hiyo anafafanua kuwa, wakikosa nafasi ya uspika, majina yao yatakuwa yamejulikana, na kwamba yawezekana mamlaka za uteuzi zikawaona na kuwateua katika nafasi nyingine za uongozi wa nchi.

"Hivyo huo ni mkakati wa kisiasa wa kujitangaza, ili kwamba hata kama watakosa, inawezekana siku moja mamlaka zikaulizia CV zao kwa lengo la kuteua miongoni mwao katika nafasi mbalimbali. Kwa hiyo ninaona wingi wao unatokana na kuchukulia kama fursa," anasema.

Anaeleza kuwa hata ikitangazwa nafasi ya katibu kata, wanaweza kujitokeza wengi kwa madai kwamba, siasa imekuwa ni ajira kwa ajili ya kutengeneza maisha bora badala ya kuzingatia weledi na vigezo na sifa za uongozi.

**WANAWAKE NI MAKINI**

Katika idadi ya makada hao wa CCM waliojitokeza kuwania uspika, wengi wao ni wanaume, huku wanawake waliochukua fomu wakiwa wachache, ambapo inaelezwa kuwa hatua hiyo inatokana na umakini wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, anasema, kwa kawaida wanawake huwa si watu wa kukurupuka, bali wanapima jambo kwanza kabla ya kufanya.

"Baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema kuwa, uongozi siyo rahisi, ni kutumikia wananchi, jipime, jihoji kwanza, lakini pia ujue maana ya uongozi, na ndivyo wanawake wanafanya," anasema Liundi.

Mkurugenzi huyo anasema, uchache wa wanawake katika kinyang'anyiro hicho, unaonyesha jinsi ambavyo si wepesi wa kukurupikia jambo, badala yake wanakaa na kutafakari kwanza kabla ya kuchukua hatua.

"Kwa uchache wao huo, ninaweza kusema kuwa wanawake si watu wa kurukia vitu, wanapeleleza kwanza ndipo wanaamua. Kwa hiyo huo ndiyo mtazamo wangu kuhusu uchache wao," anasema.

Liundi anasema, hatua hiyo ya kutojitokeza kwa wingi, pia imeonyesha ni jinsi gani wasivyo na tamaa ya madaraka, bali lengo lao ni kutumikia wananchi na siyo kutafuta maslahi binafsi. Kinamama waliojitokeza kuwania nafasi hiyo ni Dk. Tulia Ackson, Stella Manyanya, Sophia Simba.

Msururu mrefu wa wanaume miongoni mwao yumo, Andrew Chenge, Stephen Masele, Mussa Azan Zungu na Dk. Thomas Kashililah, Goodluck Mlinga, Athumani Mfutakamba, Norman Sigalla na Andrew Kevella, ambao wamejitosa kutaka kumrithi Job Ndugai aliyejiuzulu nafasi hiyo hivi karibuni baada ya kutoa madai yalipopinga na na mipango ya serikali ya kukopa fedha za maendeleo.

Ndugai alichukua hatua hiyo mwanzoni mwa mwezi huu, baada ya kuongezeka kwa shinikizo kutoka kwa viongozi mbalimbali ndani ya chama cha CCM kumtaka kujiuzulu kutokana na majibizano kati yake na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu serikali kuchukua mikopo ya maendeleo.

Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima ni miongoni mwa waliomshauri kujiuzulu nafasi hiyo kwa madai kwamba hataweza kuliongoza bunge kwa madai kwamba, wabunge wote wasingekuwa upande wake.

Naye mbunge wa Mtera mkoani Dodoma (CCM), Livingstone Lusinde, alimtaka Ndugai kuchukua hatua hiyo baada ya kujiridhisha kwa kupitia video nzima ya hotuba ya Spika Ndugai aliyoitoa katika moja ya mikutano yake na wazee uliofanyika mkoani Dodoma.



# Salamu kwako spika ujaye...

## Imarisha uvumilivu kisiasa, ukosoaji, ushauri bungeni

**Na Gaudensia Mngumi**

HARAKATI za kuwapata Spika na Naibu zinaendelea na wiki hii maandalizi yanaendelea ili kumfahamu atakayepigiwa kura mapema mwezi ujao kuliongoza bunge, baada ya Job Ndugai kujiweka pembeni.

Spika mpya anayekuja asifurahie kupata jukumu kubwa la kuongoza muhimili wa dola , bali anayelinda demokrasia bungeni sio anayetoa 'likizo' ya miezi kadhaa kwa wabunge machachari au wakosoaji bila kujali kuwa ni wajibu wao kikatiba.

Ni Spika mwenye kuonyesha na kuwa na uvumilivu wa kisiasa na wakati mwingine asiyekataa kusikiliza watu au wabunge wanaotoa mawazo ya kupinga au kutaka uwajibikaji zaidi wa serikali.

Licha ya kuliongoza bunge kwa kutumia kanuni na taratibu zinazodhibiti nidhamu ambazo bunge hilo lilizipitisha, wakati mwingine uvumilivu wa kisiasa ni muhimu kwa kuwa Watanzania wa leo wanafahamu na wanahitaji kusikia mawazo na kutaka mabadiliko badala ya kung'ang'ania kanuni kufunga wabunge midomo.

Kwa ujumla kuvumiliana si ndani ya 'ndoa' pekee kama Watanzania wengi wanavyosema lakini hata serikalini, ndani ya vyama vya kisiasa, bungeni na mitaani kati ya mashabiki wa timu kubwa kuvumiliana ni muhimu ili kuepusha mitafaruku.

Kwa upande wa bungeni ni lazima kwa sababu kuziba wabunge midomo kunaweza kuleta hisia kuwa pengine, serikali haitaki kukosolewa, ambalo ndilo jukumu la mhimili huo.

> "Bunge hilo lilikuwa liandae katiba ambayo Watanzania wangeipigia kura lilikwama na liligeuka sehemu ya kujibizana, kugombana na hata kusema siri za ndani na kunyooshea vidole, chuki ikionekana zaidi kwa mahasimu wa kisiasa.

Spika mpya atakayechukua usukani akumbuke kuwa wakati wa Bunge Maalumu la Katiba , ukosefu wa uvumilivu wa kisiasa ulidhihirika kiasi cha kukigeuza kikao hicho kuwa sehemu ya kuzungumzia hata masuala au mambo binafsi.

Bunge hilo lilikuwa liandae katiba ambayo Watanzania wangeipigia kura lilikwama na liligeuka sehemu ya kujibizana, kugombana na hata kusema siri za ndani na kunyooshea vidole, chuki ikionekana zaidi kwa mahasimu wa kisiasa.

Spika atakayepata nafasi ya kuuongoza mhimili huo wa dola ambao ni sauti ya Watanzania takribani milioni 60, asiwe mwepesi wa kuondoa hoja na mawazo ya kukosoa serikali kwa kuwa ni lazima wabunge waseme na kueleza kasoro wanazoziona ndani ya serikali.

Hii ni pamoja na uwekezaji kwenye sekta mbalimbali mfano kwenye madini, kilimo, utalii, ajira lakini pia kuzungumzia ufisadi, ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka.

Spika anapoongoza bunge akumbuke kuwa ni jukumu lake na pia ndiyo wakati kwa serikali kusikiliza mawazo ya wadau wote, wakiwamo wale wanaopinga au wanaoikosoa zaidi na wanaoleta mawazo mbadala.

Kusikiliza hoja za watu wenye fikra tofauti na njia mbadala ni utaratibu bora wa kupata maoni mengi na mbalimbali ya kujenga na kuweka mambo sawa.

Maoni hayo hasa ya wakosoaji wa sekta za uchumi, madini, usafirishaji, ujenzi wa miundombinu na kuhoji suala la kusaini mikataba mbalimbali na mienendo yake ni mambo ya kupewa nafasi sio kupingwa.

Spika mtarajiwa anatakiwa kufahamu kuwa bunge linatakiwa kuwa mfano wa sehemu iliyokomaa kwa uvumilivu wa kisiasa ili kila mmoja atoe mawazo yake kwa ajili ya kutimiza jukumu la kuisimamia, kuikosoa na kuishauri serikali kama katiba inavyoelekeza.

Siyo vibaya viongozi wa bunge na serikali kusikiliza hoja za kukosolewa na kushauriwa ili kupata mawazo mengi ambayo yatachambuliwa na kufanyiwa kazi kwa ajili ya kufanikisha maendeleo ya Tanzania.

Wakumbuke wapo katika jamii iliyo kwenye kiwango cha juu cha demokrasia na uhuru wa mawazo. Dunia ya leo ni uwanja unaoruhusu kupata maoni na fikra nyingi, michango ya mawazo ya kila aina na tofauti kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ambako mitandao ya mawasiliano ina taarifa za kila kitu na ni vigumu kuuficha ukweli.

Spika mtarajiwa ahakikishe serikali inayasikiliza, kuyachambua kama ilivyo kwa mchele na pumba au chuya ili kupata kilicho bora.

Bunge lisiwe sehemu ya kukataa maoni au mawazo bali liwe uwanja mpana wa kujua vitu vingi zaidi na namna ya kuisaidia serikali kutekeleza majukumu yake.

Bunge liwe wazi kupokea bila kudhibiti hoja au kuwashughulikia wakosoaji wakubwa ndani ya chombo hicho ili serikali ikosolewe na kushauriwa kikamilifu wakati wote.

Ni vyema pia kukumbuka kuwa Baba wa Taifa Hayati, Julius Nyerere, katika kuanzisha vyuo vikuu alisema lengo lilikuwa kupata idadi kubwa ya wakosoaji, wachambuzi wa serikali majasiri na waibuaji fikra mbadala.

Wasomi waendelee kuwa kioo cha serikali cha kujitazama wenye mawazo mbadala wayatoe na si kila mwanasiasa au msomi aunge mkono kila kitu, itakuwa ajabu na siyo makusudi ya sauti za umma kwenye kukuza demokrasia.

Hivyo si wakati wa kuzigeuza zama hizi kuwa za kukosa wakosoaji kwa sababu kila mmoja anaunga mkono kwa hofu ya kuitwa mpinzani ama anayetumiwa na wapinzani, ziwe enzi za kusema na kutetea maslahi ya taifa kwa utaratibu unaozingatia, kanuni, sheria na taratibu.

# Vita kuu ya tatu yaja, viashiria mvutano mataifa makubwa

**Na Ani Jozeni**




Marais Xi Jinping wa China, Joe Biden wa Marekani, Vladimir Putin wa Russia na Volodymyr Zelenskyy wa Ukraine mataifa yao yanashikilia hatima ya amani duniani. **PICHA MTANDAO.**

YAKO mawingu ya mvua ambayo nyakati zilizopita ingekuwa ni ishara tosha ya dhoruba ya vita inayokaribia, ila katika wakati huu hakuna taifa linaloweza kuanzisha vita kati yake na dola nyingine kubwa.

Lakini alama za nyakati ambazo ni pamoja na hisia ya kudhoofu Marekani, taifa ambalo linauchunga mfumo wa kisiasa na kiuchumi duniani tangu kumalizika Vita Vikuu vya Pili mwaka 1945.

Siyo kwamba Marekani haina silaha au mtandao wa kijeshi unaoweza kuangusha dola yoyote ile hasa kiuchumi ikitaka kuvuruga mfumo wa kimataifa uliopo iingize ubeberu, kuteka nchi na kuikalia kimabavu, bali wanahisi haitaweza kuamua hivyo kutokana na mikondo ya kutilia shaka demokrasia na mfumo wa kibepari, kutaka uporomoke.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa kwa mfano vituo vya televisheni vya CNN na Al Jazeera, wanatoa picha kuwa Marekani na Russia ziko tayari kuendelea na mazungumzo ya hatima ya Ukraine ila hakuna matarajio yoyote ya maafikiano.

Yasingeweza kuwepo, kwani madai ya Russia kuwa umoja wa kujihami nchi za Magharibi (NATO) usieneze mipaka yake mashariki (kuelekea nchi zilizokuwa sehemu ya himaya ya kijamaa ya Urusi hapo awali) hayakubaliki kwa msingi wa kuundwa kwa umoja huo. Dhamira yake ni kutetea uhuru na demokrasia kwa nchi wanachama, na kusaidia uhuru na demokrasia kwa wasio wanachama wanapotishiwa na uvamizi kutoka nje au udikteta wa ndani, na mara nyingi vinashabihiana kama ilivyojiri huko Kazhakstan. Russia na marafiki zake walipeleka vikosi kumaliza uasi wa umma jijini Almaty mji mkuu wa Kazhakstan.

Kimsingi madai ya Russia siyo rahisi kuyaelewa, kuwa wameweka zaidi ya askari 100,000 wanaotumia vifaru na mizinga mikubwa kando ya Ukraine ili kuzuia nchi hiyo kujiunga na NATO, kuwa endapo watajiunga basi wataivamia.

Sasa kinyume chake ni kukiri kuwa nchi hiyo ni 'koloni mamboleo' la Russia , kwa hiyo isijiunge, na ikishaafikiwa hivyo, maana yake ni kuwa wanachama NATO hawatahusika tena nini kitatokea huko baada ya hapo, ina maana, hata Russia ingeivamia.

Kwa hali yoyote ile, dhamira ni kuvamia kwa kisingizio cha kuzuia kujiingiza NATO, au baada ya NATO kukiri kuwa hawatajali kitakachotokea nchini humo.

Mpangilio huo wa madai wa Rais Vladimir Putin wa Russia unafanana na madai ya mwaka 1938 yaliyotolewa na mtawala wa Ujerumani Kansela Adolf Hitler, ya kuimeza Austria na kutaka kuchukua sehemu ya Czechoslovakia ambayo leo ni Jamhuri ya Check, akaruhusiwa lakini akatamani kujitwalia Poland kwa nguvu vita ikaanza.

Ni hali ambayo ipo hivi sasa katika umoja wa NATO na hasa kwa upande wa Marekani, kuwa imekataa mwelekeo wa Donald Trump, rais wa zamani wa Marekani kuhusu suala la Mashariki ya Kati na mustakabali wa makubaliano kuhusu mpango wa urutubishaji urani wa Iran, ambako Trump aliiondoa Marekani, zikabakia nchi za Ulaya.

Zimepiga kelele kuanzia wakati huo umuhimu wa kuongea na Iran na kuelewana kuhusu kutotengeneza silaha za nyuklia, huku Israeli ikipiga kelele waache kuendelea kuzungumza na Iran na kuiruhusu kutoa madai au ahadi hadaa, ikitaka iondolewe vikwazo.

Kwa upande mwingine hali si shwari Mashariki ya mbali ambako China imefuta uhuru wa habari na siasa jimboni Hong Kong uliodumu tangu jimbo hilo likabidhiwe kwake na Uingereza mwaka 1997.

Wakati hali hiyo tayari inavuruga mahusiano ya kidiplomasia na nchi za Magharibi, dhamira ya kuiteka Taiwan na kuiweka chini ya Jamhuri ya Watu wa China kijeshi iko wazi, kama ile ya Russia kuhusu Ukraine.

Tangu mwaka 1949 China imeendelea kuona Taiwan kama jimbo lake, kuwa haiwezi kuwa nchi huru kwani hadi 1949 ilikuwa nchi moja, ila serikali ya Beijing ikakimbilia Taipei pale jeshi la kimapinduzi lilipoteka mji mkuu wa Beijing.

Kanuni hiyo haibadiliki kwa China, licha ya kufikia mageuzi makubwa ya kiuchumi - ambayo hata hivyo yanateteteka kutokana na mizozo kadhaa.

> Tangu mwaka 1949 China imeendelea kuona Taiwan kama jimbo lake, kuwa haiwezi kuwa nchi huru kwani hadi 1949 ilikuwa nchi moja, ila serikali ya Beijing ikakimbilia Taipei pale jeshi la kimapinduzi lilipoteka mji mkuu wa Beijing.

Kinachowatisha kwa kiasi fulani wachambuzi - licha ya kuwa siyo rahisi kusikia mifananisho ya aina hiyo katika vyombo vya habari vya kimataifa ni kuwa ushindani uliopo na dhamira za dola za Russia na China na zinavyoisoma Marekani kuwa ni dhaifu na haiwezi tena kutetea demokrasia kama mfumo thabiti duniani, kuna fursa ambayo ikitumika vizuri inaweza kuwanufaisha Wachina na Warussia.

Ni kuondoa udhibiti kiuchumi na kijeshi wa Marekani dunia ichukue sura nyingine hivyo mitaji ya miundombinu itoke China pamoja na bidhaa takriban zote zinazohitajiwa kote duniani, wengine wakichangia kiasi wanachoweza.

Ni dunia ambayo kila nchi ingejiamulia inataka mfumo gani wa kisiasa, na siyo kulazimishwa demokrasia na haki za binadamu.

Wakati Rais Joe Biden, anaingia madarakani mapema mwaka jana, kulikuwa na viashiria vya hatari hiyo kwani alikuwa anasifiwa na kila nchi au mtawala kama mtu 'msikivu,' na anayemsikiliza kila mmoja hana msimamo thabiti kwa lolote lile kuongoza dola ya Marekani ni jambo la hatari.

Wale ambao walikuwa wanajua hawatapona endapo watakutana na ari ya Rais Trump ya kuthibitisha nafasi ya Marekani duniani na kumalizana na udikteta au makundi ya kigaidi kwa haraka na si majadiliano yasiyoisha walihisi wamepata afueni.

Iran kwa mfano imechagua rais mpya mhafidhina anayetaka Marekani iondoe vikwazo vyote ndipo mazungumzo yaanze, na Korea ya Kaskazini ambayo wakati wa Rais Trump ilifikia mahali ikalipua kinu kimoja cha kurushia makombora ya majaribio, kuihakikishia Marekani kuwa ina nia njema, ila sasa imebadilika.


Korea Kaskazini inaboresha makombora kila kukicha na kuongeza urefu wake, inajua kuwa Marekani haitafanya lolote, na jirani zake Korea ya Kusini na hata Japan 'hawaiambii lolote.'

Udhaifu huu wa kihisia wa Marekani unaotokana na upole wa kiongozi mkuu wa dola, unachochea ari mpya ya kupiga na kutawala, na endapo Japan itabadili mwelekeo wa amani inayolindwa na Marekani baada ya vita vya pili 'Pax-Americana' hali inaweza kubadilika, ikaelekea vita.

Ila Japan ilishushiwa mabomu mawili ya atomiki na Marekani mwaka 1945, na haina ari ya vita ya nyuklia, wakati Russia na China zinaonyesha nia ya mapambano na kutamani vita.

## MWANADIPLOMASIA ABDALLA HAMDOK

# Alivyowaangusha Wasudani, wakosa imani naye, ang'oka



**Na Christina Mwakangale**

NI takribani siku 16 tangu Waziri Mkuu wa zamani wa Sudan Abdalla Hamdok (pichani), kuamua kukaa pembeni baada ya kung'olewa na kurejeshwa tena kuliongoza taifa hilo. Hata hivyo aliona isiwe shida akang'atuka Januari 2, 2022, lakini bado maandamano ya kupinga utawala wa kijeshi yanatikisa mji mkuu wa nchi hiyo Khartoum.

Juzi Jumapili (Januari 16), madaktari waliandamana kupinga mashambulizi dhidi ya hospitali yanayofanywa na vikosi vya usalama wakati wa maandamano hayo ya kupinga utawala wa kijeshi na kushinikiza jeshi kurejesha uongozi wa raia.

Waziri Mkuu aliyejiuzulu, amepitia mengi ikiwamo waandamanaji kumtaka aondoke, lakini pia alikuwa katika kifungo cha nyumbani kikitanguliwa na shambulio na jaribio la mapinduzi na kutaka kuuawa nyumbani kwake, mjini Khartoum. Vyote vinaweza kuwa sababu ya kuamua kujiuzulu.

Duru za kisiasa zinasema, Hamdok sasa ameondolewa kwenye nafasi hiyo kwa maandamano ambayo yalikuwa mfululizo mjini Khartoum, waandamanaji wakidai ajiuzulu na kuitaka serikali ya kiraia, wakidai aliingia makubaliano na mamlaka ya jeshi ambayo yanaongoza nchi, ambayo si uongozi wa kiraia.

Novemba, 22 mwaka jana, Hamdok, alirejeshwa mamlakani kama sehemu ya makubaliano na jeshi kufuatia mapinduzi ya Oktoba na shinikizo la kimataifa, akiwamo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, akilaani jaribio la mapinduzi, mjini Khartoum, mwaka jana.

"Nimekuwa na heshima katika kutumikia watu wa nchi yangu kwa zaidi ya miaka miwili. Na katika kipindi hiki wakati mwingine nimefanya vizuri na kuna muda nimeshindwa," anasema Hamdok, wakati akitagaza kujiuzulu, mbele ya vyombo vya habari.

"Nilijaribu kadiri niwezavyo kuzuia nchi yetu isiingie kwenye maafa. Sasa, taifa letu linapitia mabadiliko hatari ambayo yanaweza kutishia maisha yake, isiporekebishwa haraka, " Hamdok, anasema na kuongeza kuwa juhudi zake za kuziba pengo linaloonekana kukua na kusuluhisha mizozo ya nguvu za kisiasa zimeshindwa, akionya mkwamo wa kisiasa unaoendelea tangu kutwaliwa kwa jeshi, unaweza kuwa mzozo mkubwa na kuharibu uchumi wa nchi.

Akihutubia taifa kupitia televisheni, mjini Khartoum Hamdok, anasema yafanyike mazungumzo

> "Nilijaribu kadiri niwezavyo kuzuia nchi yetu isiingie kwenye maafa. Sasa, taifa letu linapitia mabadiliko hatari ambayo yanaweza kutishia maisha yake, isiporekebishwa haraka, " Hamdok, anasema na kuongeza kuwa juhudi zake za kuziba pengo linaloonekana kukua na kusuluhisha mizozo ya nguvu za kisiasa zimeshindwa, akionya mkwamo wa kisiasa unaoendelea tangu kutwaliwa kwa jeshi, unaweza kuwa mzozo mkubwa na kuharibu uchumi wa nchi.

ili kukubaliana kuhusu mkataba wa kitaifa na kutoa dira, ili kukamilisha mpito wa demokrasia kwa mujibu wa hati ya kikatiba ya 2019 inayoongoza kipindi cha mpito.

Kuondoka kwa Hamdok madarakani ni pigo kwa ambao walitarajia mabadiliko kwa kuwa Sudan imepitia kipindi cha mpito hadi utawala wa kidemokrasia baada ya vuguvugu la wananchi lililosababisha kupinduliwa kwa rais wa muda mrefu, Omar al-Bashir mwaka 2019.

### HALI YA KIUCHUMI

Wachambuzi wa kisiasa wanaeleza kuwa juhudi za mwanauchumi, Hamdok katika kuhakikisha kunakuwa na fursa za kiuchumi nchini mwake, zinapotea, kwa kuwa alipokuwa akifanya kazi UN, alisaidia kujadili makubaliano ya nchi yake kusamehewa baadhi ya madeni ya Sudan.

Makubaliano ya Novemba, mwaka jana, yalimrejesha Hamdok kama Waziri Mkuu na kuliongoza baraza la mawaziri hadi uchaguzi ufanyike, muda mfupi baadaye, maandamano dhidi ya jeshi yalianza tena, ambayo mara nyingi yalizimwa kwa nguvu.

Maandamano yaliendelea hata baada ya Hamdok kurejea ofisini, huku baadhi ya waandamanaji wakisema kurejeshwa kwake kuli-kuwa kunasaidia kuhalalisha uongozi wa kijeshi. Marekani iliwataka viongozi wa Sudan kukomesha ghasia dhidi ya waandamanaji huku zaidi ya watu 50 wakiuawa wakati wa maandamano tangu mapinduzi. Sudan ni nchi ya tatu kwa ukubwa barani Afrika, iliyo na migogoro ya uongozi huku kukiwa na majaribio kadhaa ya mapinduzi.

### KIGOGO WA MAPINDUZI

Kiongozi wa mapinduzi Sudan, Abdel Fattah al-Burhan baada ya mapinduzi alifahamu kwamba ni chanzo cha kutengwa na jumuiya za kikanda na kimataifa, ikiwamo kuondolewa misamaha muhimu ya madeni na misaada ya kimataifa. Hakukosea Marekani ilisitisha msaada wa dola milioni 700 na mpango wa kusamehewa deni lililotokana na makubaliano na jitihada za Hamdok.

Abdel Fattah, alikuwa Mkuu wa Baraza huru la Sudan na jeshi kwenye serikali ya pamoja ya jeshi na raia hadi alipotwaa madaraka yote, alivunja baraza la mawaziri la raia, akamkataa Waziri Mkuu Abdalla Hamdok na watu wengine mashuhuri ambao jeshi lilikuwa limeafikiana nao kugawana madaraka hadi wakati wa uchaguzi mwakani.

Alionyesha wazi kutokuwa na uvumilivu na uongozi wa Hamdok, akiwa kama mtawala mwenye nguvu kijeshi, akaona anahitaji kuiokoa nchi. Wakati wa maandamano ya hivi karibuni, yaliyoungwa mkono na jeshi kwenye mji mkuu Khartoum, waandamanaji walimlaumu Hamdok kwa kudorora viwango vya maisha.

### ANACHOSIMAMIA HAMDOK

Hamdok amekuwa akilikosoa jeshi kwa kuingilia uchumi kwani linasimamia mgawo mkubwa wa bajeti, kampuni zinazomilikiwa na jeshi hazilipi ushuru na zimekumbwa na ufisadi. Kuliweka jeshi chini ya udhibiti wa raia ilikuwa ajenda kwa awamu ambayo ingefuatia kipindi ya mpito.

Wanaharakati wameshinda hatua kama hizo awali na kulazimisha jeshi kulegeza kamba hasa baada ya mauaji ya Juni 2019, makubaliano ya amani mwaka uliopita yaliyaleta makundi kadhaa yenye silaha ndani ya serikali na hakuna makubaliano yaliyofikiwa na makundi mawili makubwa ya waasi.

Huko Darfur kuna kundi la Sudan Liberation Movement linaloongozwa na Abdel Wahid al-Nur, na katika milima ya Nuba, Kordofan Kusini lipo kundi la Sudan People's Liberation Movement-North, linaloongozwa na Abdel Aziz al-Hilu.

Mwaka 2019 kufuatia harakati mbaya za jeshi kwa makundi ya waandamanaji, Marekani, Uingereza, Saudi Arabia na Milki ya nchi za Kiarabu walishinikiza kuwepo suluhu kwa njia ya mazungumzo suluhu iliyopatikana mwezi uliofuatia.



# Sera, sheria zilizopitwa na wakati kurekebishwa

**NA Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali kwa kushirikiana na wadau inapanga kufanya marekebisho ya sera na sheria zote zilizopitwa na wakati zinazohusu masuala ya maendeleo ya jamii.

Dk. Gwajima alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya kikao cha kwanza cha menejimenti ya wizara hiyo kwa waandishi wa habari.

Alisema, kikao hicho lengo lake lilikuwa ni kufanya tathmini ya mambo mbalimbali ambayo yamo katika wizara hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa tafsiri na miongozo mbalimbali.

Alisema hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan aligawa wizara hiyo pamoja na Afya ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya jamii.

Alisema kazi mojawapo ya maendeleo ya jamii ni kuhakikisha kuwa inawaunganisha wananchi pamoja na serikali yao.

"Serikali imefanya mambo mengi sana, lakini wananchi hawafahamu kuna mambo wanataka kuishirikisha serikali yao, lakini hawapati kitu cha kuwaunganisha hivyo wizara hii itahakikisha kuwa ule wajibu wa maofisa maendeleo ya jamii wanautimiza kama ilivyokuwa zamani," alisema Dk. Gwajima.

Kadhalika, alisema serikali inapanga kuwashirikisha wadau kupitia sera, sheria na miongozo ambayo imepitwa na wakati.

"Zipo sera nyingi ambazo zimepitwa na wakati kama vile ya wanawake ina zaidi ya miaka 25, lakini sera ya wazee na watoto ambazo zinahitaji kufanyia marekebisho kwa kushirikiana na wadau," alisema.

"Nampongeza sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuliona hili na kunileta mimi katika wizara hii ambayo inachangamoto mbalimbali ukitizama hapa mimi ni daktari, katibu mkuu wangu ni daktari bingwa, lakini pia naibu katibu mkuu ni mwanasheria na wizara hii ina mambo mengi sana ambayo yanahusu sheria na naibu wangu hapa ni mhasibu," alisema Dk. Gwajima.

Vile vile, alisema wizara hiyo ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha inakuwa kichocheo cha maendeleo kwa jamii na kila mtu ananufaika na fursa zilizoko nchini.

"Ili jamii iendelee pia amani na utulivu unahitajika kuwapo na maofisa maendeleo ya jamii wanatakiwa kutimiza wajibu wao kama walivyoajiriwa," alisema Dk. Gwajima.

## Watakiwa kujifunza lugha za alama kusaidia wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ILI wataalamu wa afya na ustawi wa jamii waweze kuwahudumia watu wenye ulemavu wasiosikia (viziwi) wameshauriwa kujifunza na kuielewa lugha ya alama.

Hayo yalibainishwa jana na Mratibu Mkuu wa mradi wa kuhamasisha utolewaji wa huduma za afya kwa watu wenye ulemavu, Askofu Mkuu wa Kanisa la Bethel Baptism Deaf Church of Tanzania, Frank Sarungi, jijini hapa.

Akizungumza na wataalamu wa afya na ustawi wa jamii kwenye mafunzo yaliyofadhiliwa na Shirika lisilo la kiserikali Foundition for Civil Society (FCS) yaliyofanyika jijini hapa.

Mratibu huyo alibainisha kuwa wataalamu hao wa afya na watoa huduma mbalimbali, ili waweze kufanikisha kuwahudumia kwa umakini na umahiri watu wasiosikia wanatakiwa kujifunza na kuielewa lugha ya alama.

Alisema miongoni mwa watu wenye ulemavu wakiwamo viziwi, bado kwenye baadhi ya maeneo wameshindwa kupatiwa haki zao za msingi kutokana na watoa huduma kutofahamu lugha hiyo hali ambayo inakwamisha kuwapatiwa mahitaji yao.

"Niombe sasa kwa upande wa serikali kutoa kipaumbele kwa watoa huduma mbalimbali wakiwamo madaktari, polisi, watumishi ofisini na maeneo mengineyo ya muhimu wapatiwe elimu ya kujifunza lugha hiyo ili waweze kuwahudumia kwa umakini na usahihi wasiosikia," alisema. Mratibu huyo pia aliwataka wataalamu mbalimbali wanaopata mafunzo ya elimu ya lugha ya alama kuwaelimisha wengine ili kuleta hamasa kwa wasiosikia kupatiwa huduma.

Kwa upande wao wataalamu wa afya na ustawi wa jamii wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye mafunzo hayo, walikiri kuwapo kwa changamoto hiyo kwa baadhi yao kutoifahamu lugha ya alama.

Ofisa muuguzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Proches Marandu, alisema kuwa bado kuna uhitaji mkubwa kwa wataalamu wa afya na ustawi wa jamii, wa kujifunza lugha hiyo ili waweze kutoa huduma kwa usahihi kwa watu wasiosikia.

Alisema bado kuna uhitaji mkubwa kwa wataalamu mbalimbali kujifunza na kuielewa lugha hiyo ya viziwi, ili waweze kutoa huduma kulingana na mahitaji yao wanayokabiliana nayo.

"Bado tulio watumishi wengi na watoa huduma kwenye maeneo mbalimbali, hawaifahamu lugha ya alama, hivyo nitoe rai kwa wasiofahamu lugha hiyo kuchukua hatua sasa ya kujifunza ili waweze kuwahudumia kwa usahihi zaidi," alisema.Dk. Marandu alisema wakijifunza wataweza kuwahudumia badala ya kuwahofia kama ilivyo sasa baadhi ya watoa huduma wamekuwa wakiwakwepa kutokana na kutoielewa lugha ya alama.

Alisema kuwa kutoifahamu lugha hiyo wanajiona kunyanyapaliwa na kunyimwa haki zao za msingi wanapohitaji kupata huduma mbalimbali ikiwamo ya afya.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza na wanafunzi wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Nzuguni, jijini Dodoma juzi, wakati akikagua mahudhurio ya wanafunzi kwenye siku ya kwanza baada ya kufunguliwa kwa shule zote nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Vyuo vikuu kusaidia kufundisha masomo ya sayansi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amesema mkoa una mpango wa kuvitumia vyuo vikuu vilivyoko jijini hapo kusaidia kufundisha masomo ya sayansi katika shule mbalimbali.

Mtaka, alisema hayo juzi wakati wa ziara yake katika Shule ya Sekondari ya Nzuguni, jijini hapo kwa ajili ya kukagua mahudhurio ya wanafunzi wa shule baada ya shule kufunguliwa.

Alisema mkoa una mpango wa kuvitumia vyuo vikuu vilivyoko mkoani hapo kwa lengo la kusaidia kufundisha somo ya sayansi kwenye shule.

"Hatuwezi tukawa tunalalamika kuwa tuna upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi wakati tuna vyuo vikuu, lazima tuvitumie kwa ajili ya kuinua kiwango cha elimu," alisema.

Kadhalika alisema shule zinatakiwa kuomba wanafunzi wa vyuo vikuu wanaotarajiwa kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye vyuo vikuu ili kusaidia kwenye masomo hayo.

Alivitaja vyuo vikuu vilivyoko katika Mkoa wa Dodoma kuwa ni UDOM, St. John na vyuo vya ualimu vya Bustani, Mpwapwa ambavyo vikitumika vizuri vitasaidia katika masomo hayo.

Aidha, alizitaka shule zote mkoani hapo kuendeleza vipaji vya wanafunzi walioko na wanaojiunga na shule kwa faida yao na taifa.

Mtaka, alisema kuna wanafunzi walikuwa kwenye klabu za masomo ya mazingira, rushwa na wanatakiwa kuendelezwa ili kuwa msaada kwao na jamii.

"Sio wote wanaochaguliwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu, hivyo wakiendelezwa vipaji vyao vitawasaidia kujiajiri hasa sekta ya mazingira," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Sekondari Nzuguni, Rogers Justinian, alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,600 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Justinian, alisema shule hiyo ilitarajiwa kupokea wanafunzi 583 wa kidato cha kwanza, lakini imepokea 401 katika siku ya kwanza ya kufunguliwa kwa shule bado 182 hawajafika shuleni hapo.

Alisema kuwa shule ina vyumba vya kutosha pamoja na madawati kwa wanafunzi wote walioko na wanaotarajiwa kufika kuendelea na masomo.

Alisema shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya maabara na kwa sasa kuna viwili pekee na hitaji ni zaidi ya vyumba vinne.





# Mbaroni tuhuma unyang'anyi wa kutumia silaha

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kujihusisha na matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha kama vile panga, visu na bastola.

Watu hao ni Msafiri Mwahonje (46) mkazi wa Usangu wilayani Mbarali, Boniface Shupa (36) mkazi wa Matundasi Chunya na Onesmo Mwachawi (38).

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP), Christina Musyani, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Januari 15, majira ya saa 5:00 usiku katika mji mdogo wa Makongolosi, Chunya baada ya kufanya misako inayoendeshwa na jeshi hilo.

Musyani alisema katika msako walioufanya, waliwakamata watuhumiwa hao wakiwa na silaha ambazo ni bunduki mbili, bastola moja na gobore moja zilizotengenezwa kienyeji, risasi 10 za shotgun, simu tatu za mkononi, tochi, panga na kofia mbili vyote vikitumika kufanyia uhalifu.

"Baada ya kuwakamata watuhumiwa hao na kuwahoji, walikiri kuhusika na matukio ya uhalifu likiwamo la Januari 2, mwaka huu, ambalo katika eneo la Matundasi, walivamia duka la mfanyabiashara Andreas John (22) na kuiba Sh. milioni moja na vitu vya thamani vyenye gharama ya Sh. 549,000 pamoja na kumjeruhi mke wake, Sarah Frank (21)," alisema ACP Musyani.

Musyani alisema jeshi hilo linaendelea na misako maeneo mbalimbali na kuwaomba wananchi kutoa taarifa za siri pindi wanapohisi viashiria vya uvunjifu wa amani na uhalifu ili watuhumiwa washughulikiwe kwa mujibu wa sheria.

Pia alisema jeshi hilo limejipanga kudhibiti mianya yote ya uhalifu ikiwa ni pamoja na kuyakamata magenge yote yanayohusika na njama za kuiba.




Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, ACP Christina Musyani, akionyesha kwa waandishi wa habari, bastola iliyokamatwa na jeshi hilo ikitumika kufanya uhalifu, wilayani Chunya, baada ya msako jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Kyela yapitisha bajeti Sh. bilioni 14.9

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

BARAZA la Maalum la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, limepitisha rasimu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 ya Sh. bilioni 41.9 ikiwa na vipaumbele katika sekta za afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Akizungumza katika baraza hilo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema fedha zilizotengwa katika bajeti hiyo, zitasaidia kutatua kero mbalimbali za wananchi kwa kuhakikisha vituo vya afya, ujenzi wa vyumba vya madarasa na barabara vinakamilika.

Kingamkono alisema miongoni mwa miradi inayopigiwa chapuo katika bajeti hiyo ni ujenzi wa vituo vya afya vya Ngonga, Njisi na ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja kuzunguka wilaya hiyo.

"Tunawashukuru madiwani kupitisha rasimu hii ya bajeti ambayo imesheheni masuala mbalimbali kwa maendeleo ya wilaya yetu ikiwamo matumizi ya ndani," alisema.

Mwenyekiti huyo aliwaomba wananchi kuendelea kuiunga mkono serikali katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuwa waaminifu katika ulipaji wa kodi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, alisema wilaya inamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia fedha nyingi kukamilisha miradi mbalimbali ikiwamo ujenzi wa Kituo cha Afya cha Itunge na ujenzi wa vyumba vya madarasa. Aliongeza kuwa bajeti hiyo itatimiza mahitaji ya wananchi kwa kujengewa vituo vya afya, zahanati na uboreshaji wa elimu kwa kuhakikisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia yanaboreshwa.

Pia alisema bajeti hiyo itazingatia mpango wa maendeleo kwa miaka mitano kitaifa na kimkoa sambamba na ukusanyaji wa mapato.

Magehema alisema wilaya imejipanga vyema kukusanya mapato na kuvuka lengo la mwaka jana. Katika mwaka 2021/22, walikusanya asilimia 104 na hadi sasa wamekusanya asilimia 53 ya lengo.

Alibainisha mgawanyo wa fedha za ruzuku kutoka serikali kuu kuwa ni elimu ya msingi zimetengwa Sh. milioni 631, elimu ya sekondari Sh. milioni 605, ardhi na maliasili Sh. milioni tatu.

Baadhi ya madiwani, akiwamo wa viti maalum, Tumaini Mwakatika, alisema bajeti hiyo imegusia asilimia 10 ya wanawake na vijana na kwamba kupitia fedha hizo, jitihada za wananchi kujikwamua na umaskini zitaongezeka.

## Mabilioni kujenga miundombinu mawasiliano Itigi – Kambikatoto

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetoa Sh. bilioni nane kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mawasiliano kwa wananchi wanaoishi eneo la Itigi mkoani Singida hadi Kambikatoto, Mbeya lenye ukubwa wa kilomita 265.

Kutokana na kutengwa kwa fedha hizo, serikali imewahakikishia wananchi hao kuwa watapatiwa huduma ya mawasiliano ya simu baada ya viongozi wa wizara kufanya ukaguzi wa miundombinu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Jim Yonazi, alisema juzi kuwa lengo la kukagua ujenzi wa mradi huo ni kuhakikisha unajengwa kwa viwango vinavyotakiwa na kukamilika kwa wakati ili wananchi waanze kupata huduma za mawasiliano.

"Mimi na timu yangu tumekuja eneo hilo kukagua ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ili kuona ni kwa namna gani mkandarasi ametekeleza kazi kama mkataba unavyosema. Lengo la serikali ni kuona kilio cha wana Itigi na Kambikatoto kukosa huduma ya mawasiliano kinakuwa historia," alisema Dk. Yonazi.

Alibainisha kuwa sambamba na kufanya ukaguzi wa TEHAMA pia waliangalia ujenzi wa miundombinu ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na vituo vya kuongeza nguvu ya mawasiliano.

Meneja Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu hiyo, Rajab Mikumwo, kutoka kampuni ya Raddy Fibre Solutions, alisema wanatekeleza ujenzi wa miundombinu hiyo kwa mujibu wa matakwa ya mkataba na tayari nyaya zimelazwa ardhini na katika baadhi ya maeneo. Aliongeza kuwa baadhi ya nyaya pia zimepitishwa juu ya nguzo kuendana na jiografia ya eneo husika endapo kuna mto au mwamba ili kuhakikisha mawasiliano yanapatikana kwa uhakika mwanzo hadi mwisho wa eneo husika.

Mkurugenzi wa TEHAMA wa Wizara hiyo, Mulembwa Munaku, alisema tayari serikali imefikisha miundombinu hiyo kwenye maeneo ya mipaka ya nchi za jirani zinazopakana na Tanzania na sasa hatua zinaendelea kufikisha mawasiliano hayo mpakani mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Tanzania ili nchi jirani ziendelee kutumia na kunufaika na miundombinu hiyo.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Miundombinu ya TEHAMA wa Wizara hiyo, Mhandisi Nikusubila Michael, alisema ujenzi wa miundombinu hiyo utawezesha watoa huduma za mawasiliano nchini kufikisha huduma za mawasiliano kwa wananchi kwa kuwa tayari watoa huduma hao wamewasilisha mahitaji hayo wizarani.

Ujenzi wa miundombinu hiyo utaongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA kwa taasisi za serikali, sekta binafsi na wananchi walio kwenye maeneo hayo ambapo miundombinu hiyo imejengwa.





# Kampuni UAE kuwekeza Zanzibar

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameshuhudia utiaji saini wa miradi mikubwa ya uwekezaji baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya Eagle Hills Regional Properties ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Utiaji saini huo kwa upande wa Zanzibar, ulifanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Shariff Ali Shariff, na kwa upande wa Eagle Hills Regional Properties ulifanywa na Mohammed Ali Rashid Alabar. Mwekezaji huyo awali alimweleza Rais Dk. Mwinyi kuridhishwa kwake na mazingira ya uwekezaji Zanzibar tofauti na alivyotembelea katika mataifa mengine duniani ambako nako amewekeza miradi mikubwa.

Alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais Dk. Mwinyi kwa kumuunga mkono na kuahidi kwamba atafanya kila linalowezekana kuhakikisha uwekezaji anaotarajia kuufanya unafanikiwa.

Miradi inayotarajiwa kujengwa na mwekezaji huyo ni hoteli ya nyota tano eneo la Kizingo, mjini Zanzibar. Mwekezaji huyo anatarajiwa pia kujenga nyumba Zanzibar kwa ajili ya makazi. Chini ya mradi huo, eneo lingine litakalonufaika na uwekezaji huo ni Matemwe katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ambako kutajengwa hoteli yenye hadhi ya nyota tano pamoja na nyumba za kuishi zenye hadhi ya juu kwa ajili ya soko la watalii na watu wenye uwezo.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alihudhuria sherehe za kuwatunuku vyeti washindi wa mpango endelevu wa Abu Dhabi unaojikita kuendeleza masuala ya afya, chakula, nishati, maji na maendeleo ya elimu duniani katika sherehe iliyofanyika Dubai.

Rais Dk. Mwinyi katika shughuli nyingine aliyoifanya ni kutembelea banda la Tanzania katika maonyesho ya Kimataifa ya Dubai yanayojulikana kama 'Expo 2020'.

Rais Dk. Mwinyi anaendelea na ziara yake katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), ziara inayotarajiwa kumalizika leo na kurejea Zanzibar.

## Mil. 100/- zatumika ununuzi wa karafuu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, amesema serikali imetumia zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya ununuzi wa karafuu kwa msimu ulioanza mwaka jana.

Aliyasema hayo mjini Zanzibar jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya wizara hiyo.

Waziri alikiri kuwa licha ya Pemba kuzalisha kiwango kikubwa cha karafuu kilinufaishwa na Unguja, bado maisha ya wananchi wa kisiwa hicho ni duni.

Alisema wananchi wengi kisiwani humo hawamiliki mashamba ya karafuu na hunufaika na shughuli za uchumaji au uanikaji wa karafuu.

"Mashamba mengi ya karafuu huwa yanamilikiwa na serikali au watu binafsi ambao hawaishi Pemba, hivyo fedha wazozipata kutokana na karafuu, mzunguko wa fedha hautumiki Pemba," alisema.

Alisema fedha hizo zingekuwa zinatumika Pemba kwa ajili ya kutengeneza ajira, maisha ya wananchi wa Pemba yangebadilika.

Pia alisema serikali imejipanga kuifanya Pemba kuwa eneo maalum la uwekezaji ili kuitoa katika umaskini wa kipato.

Alieleza tayari imeshakaribisha wawekezaji mbalimbali kuwekeza Pemba ikiwamo kujenga viwanda. Hivi karibuni viwanda viwili vimefunguliwa kikiwamo cha maji na vinywaji baridi.

**"Mashamba mengi ya karafuu huwa yanamilikiwa na serikali au watu binafsi ambao hawaishi Pemba, hivyo fedha wazozipata kutokana na karafuu, mzunguko wa fedha hautumiki Pemba," alisema.**



Wanafunzi wa mwaka wa tatu wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), wakiwa katika mafunzo kwa vitendo kuhusu usanifu wa majengo ya kale, visiwani Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanafunzi Ardhi wajifunza kwa vitendo ujenzi majengo ya kale

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI wa mwaka wa tatu wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), wako visiwani Zanzibar kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kuhusu majengo ya kale.

Akizungumza jana na Nipashe, Mhadhiri Msaidizi wa chuo hicho, Richard Moses, alisema hiyo ni moja ya sehemu za ufundishaji wa chuo inayohusisha kuwanoa wanafunzi kwa njia ya vitendo.

Alisema wanafunzi hao 50 wanaosomea shahada ya usanifu majengo watakaa visiwani humo kwa siku 14 wakijifunza masuala ya usanifu.

Ingawa wanafunzi hao wanasomea usanifu kwa majengo mapya, pia alisema wanalazimika kupata ujuzi kuhusu majengo ya kale kwa kuyapima na kuyarekodi ukubwa wa majengo na yalitumikaje.

"Wanachunguza majengo haya yalipitia matumizi gani mpaka leo hii na pia watapendekeza mabadiliko ambayo yanapaswa kufanywa kwa majengo hayo ili yaendelee kutumika kwa miaka mingi, hivyo watajifunza kwa vitendo kuhusu majengo ya kale," alisema mhadhiri huyo.

Alisema lengo kubwa hasa la kuwapeleka visiwani Zanzibar ni kuwajengea uwezo wa kukabiliana na soko la ajira kwa kujua masuala mbalimbali kwa vitendo, hivyo kuwaongezea ujuzi.

"Wakiwa hapa Zanzibar wanafunzi hawa wamefanya tathmini katika Mji Mkongwe, maarufu kama Stone Town kwa kupata historia yake, matumizi ya jengo wakati wa zamani na sasa, aina ya ujenzi uliotumika, thamani, na vipimo mbalimbali kwa kuendana na wakati husika," alisema.

Alisema pamoja na hilo taarifa hizo zinaweza kusaidia kutumika na wataalamu mbalimbali hasa kwenye kushauri au kupendekeza juu ya matumizi, thamani na matumizi endelevu ya majengo hayo kongwe kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

## HABARI KIMATAIFA

# Wakenya wahofia miili iliyotupwa mtoni

**Nairobi,** KENYA

WAKENYA kupitia mtandaoni wamekuwa wakielezea kushtushwa na kughadhabishwa kwao, kufuatia ripoti za kupatikana kwa miili iliyotupwa kwenye mto katika eneo la magharibi mwa nchi hiyo.

Mwanaharakati Boniface Mwangi ameandika kwenye Twitter kwamba, yeye na mkuu wa Shirika la Kutetea Haki la Afrika, wamehesabu zaidi ya miili 20 iliyooza katika chumba cha kuhifadhi maiti katika Hospitali ya Yala.

**Hatukumwamini, lakini tulikubali kuandamana naye hadi mtoni. Ndani ya dakika moja, alikuwa ameona na kutuonyesha maiti mbili.**

Alisema miili hiyo, iliyopatikana katika Mto Yala, iliorodheshwa kama wanaume wasiojulikana baadhi ikiwa na alama ya kuteswa na kufungwa kwa kamba.

Wakazi wa eneo hilo, waliohojiwa walisema wameopoa miili 31 kutoka kwenye mto huo, kuanzia Julai mwaka jana na kuongeza kwamba bado kuna miili zaidi kwenye mto.

"Hatukumwamini, lakini tulikubali kuandamana naye hadi mtoni. Ndani ya dakika moja, alikuwa ameona na kutuonyesha maiti mbili. Mazingira ya eneo hilo yanasikitisha sana," mwanaharakati huyo aliandika.

Wakazi wa eneo hilo, wanaripotiwa kusema kwamba, miili hiyo inaletwa kutoka maeneo tofauti ya nchi ikiwa ndani ya gari na kutupwa mtoni.

Wakenya wanataka uchunguzi kufanywa, ili kutambua waliofariki na kubaini ni nani aliyehusika na mauaji hayo. Pia wametoa wito kwa polisi kuwahakikishia usalama wao. **BBC**



Waandamanaji wakiandamana mji mkuu wa Sudan, Khartoum ikiwa ni mwendelezo wa maandamano katika miji tofauti ya nchi hiyo, hadi jana vikiarifiwa vifo 71 tangu Oktoba mwaka jana, yalipoanza maandamano. **PICHA: DW**

## Waandamanaji saba wadaiwa kuuawa na vikosi vya usalama

**Khartoum,** SUDAN

VIKOSI vya usalama Sudan, vinadaiwa kuwaua waandamanaji saba, baada ya kuwafyatulia risasi waandamanaji dhidi ya maandamano ya kupinga mapinduzi ya kijeshi.

Ghasia za Jumatatu, wiki hii ambazo zimetokea kwenye mji mkuu wa Sudan, Khartoum na kwenye miji mingine mikubwa, zimefanyika kabla ya ziara ya wanadiplomasia wa Marekani.

Marekani inajaribu kusaidia kuumaliza mzozo uliodumu kwa miezi kadhaa kwenye taifa hilo la Afrika Kaskazini.

Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa, Volker Perthes, amelaani kile alichokiita matumizi ya risasi za moto kwa lengo la kuzuia maandamano.

Alisema takriban watu saba, wameuawa na wengine kadhaa wamejeruhiwa, huku ubalozi wa Marekani mjini Khartoum ukikosoa mbinu za kuzuia ghasia zinazotumiwa na vikosi vya usalama vya Sudan.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, liliitaka Serikali ya Sudan kujizuia kutumia nguvu dhidi ya waandamanaji.

Wanachama tisa wa baraza hilo, ikiwamo Uingereza na Ufaransa, walitoa wito huo, wakisisitiza kuhusu umuhimu wa kukusanyika kwa amani na uhuru wa kujieleza.

Vifo saba vilivyotokea Jumatatu, wiki hii, vinaifanya idadi ya watu waliouawa katika maandamano kufikia 71 tangu jeshi lilipofanya mapinduzi Oktoba 25, mwaka huu, yaliyoongozwa na Jenerali Abdel Fattah al-Burhan.

Wiki hii, madaktari wanaopinga mapinduzi na kutetea demokrasia, walisema waandamanaji watatu waliuawa kwa kupigwa risasi na wapiganaji wa baraza la kijeshi na baadaye Kamati Kuu Huru ya Madaktari wa Sudan, iliripoti kuhusu watu wengine wanne, waliouawa wakati wa mauaji hayo yaliyotekelezwa na maofisa waliofanya mapinduzi.

Mmoja wa waandamanaji, Hamed al-Ser alisema wanaandamana kupinga udhalimu, udikteta na utawala wowote unaokwenda kinyume na uhuru wa watu au haki yao.

"Niko hapa leo kwa sababu ninapinga mapinduzi ya kijeshi. Tuna matumaini harakati zetu zitafanikisha kuwapo utawala wa kiraia unaozingatia kidemokrasia na hatimaye watu wa Sudan, watafikia malengo yao yote," alisisitiza Hamed. **DW**

## ILO: Ajira itakua kwa kasi ndogo

**Geneva,** USWISI

SHIRIKA la Kazi la Duniani (ILO), limeonya mwaka 2022, sekta ya ajira inatarajiwa kukua taratibu na tena bila uhakika kutokana na kuendelea kuwapo kwa janga la Covid-19, ambalo limeathiri soko la nguvukazi duniani.

Ripoti mpya ya ILO, kuhusu Mtazamo wa Ajira Duniani (WESO), iliyotolewa juzi mjini Geneva, ilieleza kwamba, kupungua huko kumetokana na kuendelea kuibuka kwa aina mpya za virusi vya Covid-19, Delta na Omicron.

Ripoti hiyo, inaonya juu ya utofauti mkubwa katika athari baina ya makundi ya wafanyakazi pamoja na nchi.

Tofauti hizo zinazidisha kukosekana kwa usawa ndani ya nchi baina ya hali inayodhoofisha mfumo wa kiuchumi, kifedha na kijamii wa takriban kila taifa, bila kujali maendeleo.

Uharibifu huo, una uwezekano wa kuhitaji miaka mingi kurekebishwa, kwa kuhitaji ushiriki mkubwa wa wafanyakazi, mapato ya kaya na kijamii pia uwepo wa utashi wa kisiasa. **UN**

## Alpha Conde afuata matibabu ughaibuni

**Kinshasa,** DRC

RAIS wa zamani wa Guinea, Alpha Conde, aliyepinduliwa madarakani Septemba, mwaka jana, amepanda ndege kwenda nje ya nchi kwa uchunguzi wa kitabibu, vyanzo viwili vilisema, bila kueleza anakokwenda.

Mwezi uliopita, utawala wa Junta, ulisema rais huyo wa zamani ataruhusiwa kusafiri kwa misingi ya matibabu, ingawa matibabu yake yasizidi mwezi mmoja.

Chanzo cha karibu na rais huyo, kilisema alipanda ndege saa mbili usiku, juzi. Ofisa Mkuu wa Serikali, alithibitisha kuwa ameondoka.

Mapinduzi ya Septemba, mwaka jana, yalilaaniwa na majirani wa nchi ya Guinea na washirika wa kimataifa na kusababisha kuondolewa Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Kiuchumi ya Kikanda ya Afrika Magharibi (ECOWAS). **REUTERS**

HABARI MICHEZO

# KOCHA MBEYA CITY ATOA SIRI USHINDI DHIDI YA SIMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, amesema bado anaendelea kuwajenga kimbinu wachezaji wake ili kuweza kupata matokeo mazuri kwenye michezo iliyopo mbele yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema ushindi wao dhidi ya Simba ni mwanzo tu na kwamba bado hawajamaliza hivyo hauwezi kuwafanya kubweteka na kujiona wako bora.

Alisema hawataishia kwa Simba tu kupata matokeo chanya kwani lengo lake ni kuhakikisha anaendelea kufanya kazi ya kukiimarisha kikosi chake ili kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao.

"Nina kazi kubwa kuongeza kitu kwa wachezaji wangu kwa sababu tunahitaji kuchafua watu msimu huu, nawapongeza wachezaji wangu kwa kufanya kile nilichowaelekeza na kupata ushindi dhidi ya Simba," alisema Lule.

Alisema siri kubwa ya kupata matokeo mbele ya Simba ni baada ya kukaa na wachezaji wake kuwajenga kisaikolojia na kuwaeleza wanaweza kupambana na mpinzani yeyote.

"Niliwataka wasiwe na presha juu ya majina ya wachezaji na viwango wala maslahi kwa sababu wanaweza kufanya kitu na wamefanya kile nilichowaeleza na kufanikiwa kupata ushindi huo," alisema Lule.

Alisema mbali na kuwajenga kisaikolojia wachezaji wake pia waliangalia jinsi Simba inavyocheza ubora na mapungufu ya wapinzani wao hao na kufanikiwa kupata pointi tatu nyumbani.

"Tumefanya 'scouting' kila mechi, tuliwafuatilia Simba na tumefanikiwa kuziba katika njia zote na hatimaye kufanikiwa kuondoka na alama muhimu katika mchezo huo," alisema kocha huyo.

Alisema atahakikisha wanapata muendelezo mzuri wa matokeo katika mechi zao zijazo ili kuhakikisha wanamaliza ligi hiyo wakiwa katika nafasi ya tatu ambayo wako nayo sasa.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi, Mbeya City ilishinda 1-0, shukrani zikimwendea Paul Nonga aliyeifungia bao hilo pekee.

# Vivier aahidi kuipasha Biashara United

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Biashara United, Vivier Bahati, ameanza kazi rasmi ya kukinoa kikosi hicho huku akiweka wazi kwamba lengo lake ni kuhakikisha anapambana ili kuiwezesha timu hiyo kufanya vizuri na kuendelea kuwa tishio katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Vivier, ambaye alikuwa Kocha Msaidizi wa Azam FC, kwa sasa amekabidhiwa jukumu la kukinoa kikosi cha Biashara United akichukuwa nafasi ya Patrick Odhiambo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema wamemalizana na uongozi wa Biashara United na sasa kazi yake kubwa ni kukinoa kikosi hicho ili kupata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao.

Alisema amekuta timu ikiwa katika nafasi ya 15 ya pili kutoka mwisho baada ya kujikusanyia pointi 10 katika michezo 12 waliyocheza, hivyo lengo lake ni kuhakikisha wanapambana kutafuta ushindi ili kutoka katika nafasi hiyo.

"Ligi imekuwa ngumu, nina imani tutatoka katika nafasi hii tuliyopo sasa kwa kuhakikisha tunapambana kutafuta matokeo chanya katika kila mechi iliyopo mbele yetu ili kujinasua tulipo sasa," alisema Vivier.

Alisema ana imani na wachezaji wake, na kwamba tayari ameongea nao baada ya kukabidhiwa majukumu ya kukinoa kikosi hicho rasmi, jambo ambalo anaamini watafanikiwa katika malengo yao ya kutafuta pointi katika kila mechi.

"Kulingana na ligi ilivyo, yeyote anayeshida anapanda nafasi ya juu na tunatarajia kuona hilo katika michezo yetu ijayo, ukipoteza unashuka chini kitu ambacho hatutaki kuona kikijitokeza kwetu, tutapambana kupata matokeo chanya," alisema Vivier.

Biashara United haikuanza vizuri msimu huu na iko katika nafasi ya 15 ikiwa juu ya Kagera Sugar inayoshika mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.




Kiungo wa Azam FC, Ibrahimu Ajibu, akimiliki mpira katika mazoezi ya mwisho juzi jioni katika Uwanja wa FFU jijini Mbeya kabla ya jana kushuka dimba la Sokoine kuivaa Mbeya Kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: AZAM FC**

# Mtibwa Sugar yatambulisha straika mpya Mganda

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ikijiandaa kukaribisha Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaopigwa Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro Jumamosi wiki hii, Klabu ya Mtibwa Sugar imemtambulisha rasmi straika mpya kutoka Uganda, Brian Mayanja.

**Katika taarifa fupi iliyotolewa kupitia mitandao ya kijamii ya klabu hiyo huku ikiambatana na picha ya mshambuliaji huyo baada ya kukabidhiwa jezi ya Mtibwa Sugar, ilisomeka: " Tunayo furaha kumtambulisha kwenu mshambuliaji wetu mpya, Brian Mayanja kutoka timu ya Polisi Uganda."**

Usajili huo utakuwa umemulika eneo muhimu katika kikosi hicho ambacho kimeshuka dimbani mara 12 msimu huu na kuambulia pointi 11 kutokana na kushinda mechi mbili, sare tano na kupoteza michezo mitano, hivyo kukaa katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

Katika mechi hizo, Mtibwa imefunga mabao saba na kuruhusu 10, hivyo usajili wa Mayanja unatarajiwa kuongeza idadi ya mabao katika safu ya ushambuliaji.

Katika mechi ya Jumamosi, Mtibwa Sugar itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kutoka kuambulia sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Ruvu Shooting huku wageni zao, Simba nao wakitoka kujeruhiwa kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu msimu huu baada ya juzi, Jumatatu kukubali kichapo cha bao 1-0 katika Uwanja wa Sokoine dhidi ya Mbeya City.

Licha ya Simba kupoteza mchezo huo, bado ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na alama 24, nane nyuma ya vinara Yanga waliopo mchezo mmoja mbele

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MARTIAL HATAKI MKOPO
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26, anataka kuondoka Manchester United, lakini si kwa mkopo kwenda klabu nyingine ya England. Barcelona, Sevilla na Juventus ndizo klabu tatu anazopigiwa upatu wa kujiunga nazo katika uhamisho huu wa Januari. ***(Fabrizio Romano)***

### MCGINN AWANIWA UNITED
KLABU ya Manchester United inamnyatia kiungo wa kati wa Aston Villa na Scotland, John McGinn mwenye umri wa miaka 27, katika uhamisho wa msimu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### BARISIC AGOMBEWA
MLINZI wa Rangers, Borna Barisic mwenye umri wa miaka 29, amethibitisha kuwa kuna klabu iliyowasilisha ombi la kumnunua awali katika dirisha la uhamisho, licha ya tetesi zinazomhusisha kiungo huyo wa kimataifa wa Croatia na Watford na Aston Villa. ***(Sky Sports)***

### MELO HAKIELEWEKI ARSENAL
MAZUNGUMZO ya Arsenal na Juventus kuhusu mkataba wa mkopo wa kiungo, Arthur Melo yamekwama kwa sababu klabu hiyo ya Serie A bado haijapata mbadala wa Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Tuttomercatoweb, via Express)***

### TCHOUAMENI KUTUA CHELSEA
CHELSEA huenda ikapewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Monaco, Mfaransa Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21, huku Manchester United wakielekeza darubini yao kwa kiungo wa RB Leipzig na Mali, Amadou Haidara, 23, na kiungo wa Borussia Monchengladbach na Uswisi mwenye umri wa miaka 25, Denis Zakaria. ***(Football.london)***

### COSTA KUUNGANA NA WILLIAN
DIEGO Costa mwenye umri wa miaka 33, ambaye anahusishwa na Arsenal, anataka kuhamia klabu ya Brazil ya Corinthians, ambako huenda akaungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Chelsea, Willian. ***(Evening Standard)***

### MILINKOVIC-SAVIC ANUKIA MAN
MANCHESTER United ipo mbele ya Juventus na Inter Milan katika mbio za kumsaka kiungo wa kati wa Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 26 kutoka Lazio. ***(Il Messaggero via Sport Witness)***

### HAZARD ATAKA KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Eden Hazard anataka kuondoka Real Madrid, lakini hana mpango wa kujiunga na Newcastle, ambao walikuwa wamewasilisha dau la pauni milioni 41.3 kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. ***(El Nacional)***

### DEMBELE APEWA SAA 48
BARCELONA imempa winga wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, Ousmane Dembele saa 48 kuamua kuhusu mkataba mpya aliyopewa na klabu hiyo. ***(Mundo Deportivo)***

### CHELSEA YAITIWA KURZAWA
KLABU ya Paris St-Germain imewapa Chelsea nafasi ya kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Layvin Kurzawa, lakini kocha, Thomas Tuchel hamtaki mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Goal)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI AMFUNIKA MESSI, SALAH TUZO ZA FIFA

Ronaldo yeye apewa tuzo maalumu, Tuchel, Edouard Mendy nao wang'ara na kubeba...

**NYON, Uswisi**

STRAIKA wa Bayern Munich na Poland, Robert Lewandowski, ametawazwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa) kwa mwaka 2021, huku nyota wa Manchester United, Cristiano Ronaldo akitunukiwa tuzo maalumu.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, alitwaa tuzo hizo kwa mara ya pili mfululizo baada ya kufunga mabao 69.

Alishinda mbele ya straika wa Liverpool, Mohamed Salah na nyota wa Paris St-Germain, Lionel Messi.

Ronaldo alitwaa tuzo maalumu baada ya kuwa mfungaji bora wa wakati wote kwenye mechi za kimataifa kwa wanaume.

Mchezaji wa Barcelona, Alexia Putellas alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka kwa upande wa wanawake.

Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel alishinda tuzo ya kocha bora wa mwaka baada ya kuisaidia Chelsea kubeba taji la pili la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kujiunga na klabu hiyo Januari mwaka jana.

Mchezaji wa zamani wa Tottenham Hotspur, Erik Lamela - ambaye aliuzwa kwenda Sevilla kipindi cha majira ya joto - alitwaa tuzo ya Fifa Puskas, kwa kufunga bao bora la msimu dhidi ya Arsenal Machi mwaka jana.

Golikipa wa Chelsea, Edouard Mendy alitwaa tuzo ya kipa bora wa mwaka baada ya kuisaidia timu yake kubeba ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati walipoifunga Manchester City bao 1-0.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 861,

MECHI KALI
BRENTFORD
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 4.04
X | 3.56
2 | 1.88

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARTINEZ ATAJWA KUWANIWA EVERTON



**LIVERPOOL, England**

BAADA ya kumtimua Rafa Benitez, Klabu ya Everton ipo kwenye mchakato wa kumpata kocha wa kuiongoza timu hiyo huku jina la Roberto Martinez likitajwa zaidi.

Martinez si jina geni miongoni mwa mashabiki na wadau wa Everton kwani aliwahi kuwa kocha wa klabu hiyo na kuifikisha nafasi ya tano kabla ya kufululiza kumaliza misimu miwili kwenye nafasi 11.

Nafasi ya tano ni kubwa na ya mafanikio kwa klabu hiyo kuipata kwenye muongo mmoja uliopita.

Safari hii, hali ni mbaya zaidi wanaelekea katika nafasi zenye hatari ya kushuka daraja, licha ya kufanya usajili mkubwa mwanzoni na katikati ya msimu huu.

Benitez alitupiwa virago baada ya kufanya kazi kwa siku 200 pekee katika klabu hiyo.

Kwa mujibu wa BBC Sport, uongozi wa 'Toffees' hao umeanza hatua za awali za kumtoa Martinez kwenye kibarua chake cha kuiongoza timu ya Taifa ya Ubelgiji.

Wayne Rooney, Frank Lampard na Duncan Ferguson ni miongoni mwa majina yanayohusishwa na kibarua hicho kule Goodison Park.

# Aubameyang ruksa kurudi Arsenal

**LONDON, England**

KOCHA wa timu ya Taifa ya Gabon amemruhusu mshambuliaji wake, Pierre-Emerick Aubameyang kuondoka kwenye michuano ya Afcon na kurudi klabuni kwake ili aende akajiuguze baada ya kupata maambukizi ya corona.

Vyombo mbalimbali vimeripoti kuwa alipewa ruhusa kutokana na kuwa na matatizo ya moyo, lakini kocha wa timu hiyo hakuweza kuzungumzia suala hilo na kusema kuwa ulikuwa uamuzi sahihi tu kumruhusu Aubameyang.

Kocha Patrice Neveu pia amemruhusu kiungo anayecheza Ufaransa, Mario Lemina ambaye karudi kwenye timu yake ya Nice ambapo hakuweza kucheza hata dakika moja kwenye michuano hiyo.

"Tumefanya maamuzi sahihi kuwarudisha kwenye klabu zao, wanaweza kuangaliwa vizuri wakiwa kule," alisema kocha Neveu akiwaambia waandishi wa habari.

Mchezaji huyo hajafanikiwa kucheza mchezo wowote kwenye michuano hiyo inayoendelea nchini Cameroon ambapo kwa sasa inaelekea hatua ya mtoano kuelekea nusu fainali na fainali.



636,800

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/01/22 | 18:00 | Zaragoza vs Valladolid | 2.94 | 3.08 | 2.41 |
| 02. 22/01/22 | 18:30 | Moreirense vs Santa Clara | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 03. 22/01/22 | 20:15 | Fuenlabrada vs Las Palmas UD | 2.99 | 3.04 | 2.40 |
| 04. 22/01/22 | 21:00 | Tondela vs FC Vizela | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 05. 22/01/22 | 23:00 | Malaga vs UD Ibiza Eivissa | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 06. 23/01/22 | 16:00 | Granada vs Osasuna | 2.51 | 3.16 | 2.91 |
| 07. 23/01/22 | 16:00 | Burgos vs Leganes | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 08. 23/01/22 | 16:00 | Giresunspor vs Alanyaspor | 2.63 | 3.18 | 2.63 |
| 09. 23/01/22 | 19:00 | Galatasaray vs Trabzonspor | 2.55 | 3.19 | 2.70 |
| 10. 23/01/22 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.80 | 2.95 | 2.75 |
| 11. 23/01/22 | 22:00 | Waalwick vs Fortuna Sittard | 2.32 | 3.35 | 2.85 |
| 12. 23/01/22 | 22:45 | AC Milan vs Juventus | 2.66 | 3.26 | 2.66 |
| 13. 23/01/22 | 23:00 | Alcorcon vs Mirandes | 2.65 | 3.09 | 2.65 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**JUMATANO - 19/01/2022**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4605 | Karmiotissa vs Onisilos Sotira FC | 2.25 | 3.12 | 2.98 |
| 15:00 | 3691 | Peterborough United Reserve vs Sheffield Wednesday U23 | 1.78 | 4.10 | 3.95 |
| 16:00 | 1009 | Panathinaikos B vs O F Ierapetras | 2.36 | 3.22 | 2.74 |
| 16:00 | 2518 | Almopos Arideas vs Niki Volou | 3.37 | 3.13 | 2.06 |
| 16:00 | 2623 | Volos vs Apollon Smyrnis | 1.74 | 3.64 | 4.43 |
| 16:00 | 2659 | AEK Athens B vs Egaleo Athens | 2.65 | 2.89 | 2.65 |
| 16:00 | 2935 | Panetolikos vs Olympiakos | 7.73 | 4.64 | 1.32 |
| 16:30 | 3389 | EN Paralimni vs Ermis Aradippou | 1.81 | 3.27 | 4.14 |
| 17:00 | 1022 | Goeztepe vs Sivasspor | 2.44 | 3.19 | 2.85 |
| 17:00 | 1403 | Kayserispor vs Basaksehir | 3.21 | 3.31 | 2.17 |
| 17:00 | 2194 | FC Goa vs East Bengal | 1.55 | 4.06 | 4.83 |
| 17:00 | 3997 | Caykur Rizespor vs Antalyaspor | 2.60 | 3.28 | 2.60 |
| 17:30 | 1015 | Pafos FC vs Anorthosis Famagusta | 2.55 | 3.08 | 2.60 |
| 18:00 | 5114 | Panathinaikos vs Anagennisi Karditsas | 1.20 | 5.60 | 11.59 |
| 19:30 | 1877 | Oliveirense vs CDC Montalegre | 1.71 | 3.51 | 4.33 |
| 19:30 | 3307 | Sassuolo vs Cagliari | 1.62 | 4.05 | 4.74 |
| 20:00 | 3298 | Trabzonspor vs Giresunspor | 1.61 | 3.85 | 5.14 |
| 20:00 | 3572 | Fenerbahce vs Altay | 1.37 | 4.83 | 7.29 |
| 20:00 | 4565 | PAOK vs AEK Athens | 2.23 | 3.14 | 3.00 |
| 20:00 | 5971 | Apoel Nicosia vs Olympiakos Nicosia | 1.79 | 3.33 | 4.16 |
| 20:30 | 3526 | Hannover vs Monchengladbach | 4.69 | 4.19 | 1.65 |
| 20:30 | 5269 | RB Leipzig vs Hansa | 1.10 | 9.23 | 22.07 |
| 20:45 | 2434 | Groningen vs NEC Nijmegen | 2.19 | 3.13 | 3.09 |
| 21:00 | 2931 | Amiens vs AC Ajaccio | 3.10 | 2.96 | 2.38 |
| 21:00 | 3279 | Celta Vigo vs Osasuna | 1.88 | 3.40 | 4.29 |
| 21:00 | 3784 | Lille vs Lorient | 1.52 | 4.19 | 5.99 |
| 21:00 | 4081 | Clermont Foot vs Strasbourg | 3.04 | 3.39 | 2.27 |
| 21:00 | 4612 | Montpellier vs Troyes | 1.74 | 3.83 | 4.37 |
| 21:00 | 5321 | Toulouse vs Nancy | 1.47 | 4.22 | 6.09 |
| 21:15 | 5980 | America SE vs Boca Junior SE | 2.79 | 3.37 | 2.24 |
| 22:00 | 1777 | Guinea Bissau vs Nigeria | 4.96 | 3.62 | 1.69 |
| 22:00 | 2023 | Egypt vs Sudan | 1.23 | 5.18 | 14.94 |
| 22:00 | 5126 | NAC Breda vs PEC Zwolle | 2.93 | 3.17 | 2.25 |
| 22:30 | 4696 | Leicester vs Tottenham | 2.96 | 3.37 | 2.35 |
| 22:45 | 1269 | Hoffenheim vs SC Freiburg | 2.06 | 3.70 | 3.30 |
| 22:45 | 2514 | Racing Genk vs Mechelen | 1.53 | 4.44 | 5.13 |
| 22:45 | 4393 | Tiverton Town vs Yate Town | 2.60 | 3.71 | 2.24 |
| 22:45 | 4542 | Hertha BSC vs Union Berlin | 2.66 | 3.26 | 2.66 |
| 22:45 | 5136 | Gosport Borough vs Hayes Yeading United | 2.73 | 4.12 | 2.03 |
| 22:45 | 5157 | Cray Wanderers vs Leatherhead | 1.71 | 3.96 | 3.81 |
| 22:45 | 5797 | Hull City vs Blackburn | 2.99 | 3.18 | 2.32 |
| 23:00 | 1154 | Twente vs AZ Alkmaar | 3.28 | 3.23 | 2.06 |
| 23:00 | 1173 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.83 | 3.07 | 2.53 |
| 23:00 | 1339 | Brentford vs Manchester Utd | 4.04 | 3.56 | 1.88 |
| 23:00 | 1353 | Reading vs Luton Town | 3.53 | 3.38 | 2.00 |
| 23:00 | 1653 | CSD Camara De Lobos vs Limianos | 3.81 | 3.23 | 1.89 |
| 23:00 | 2750 | Birkirkara vs Balzan Youths | 2.23 | 3.50 | 3.05 |
| 23:00 | 4876 | Lugo vs Almeria | 3.29 | 3.19 | 2.16 |
| 23:00 | 5241 | Inter vs Empoli | 1.23 | 6.33 | 9.89 |
| 23:30 | 1525 | Valencia vs Sevilla FC | 3.19 | 3.14 | 2.34 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DAR CITY YAITEGA SIMBA FA CUP

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupangwa dhidi ya Mabingwa Watetezi wa Kombe la FA, timu ya Dar City iliyoko Daraja la Kwanza Tanzania Bara, imesema imefurahi kucheza na miamba hiyo na itajifunza mechi kutoka kwao.

Rais wa klabu hiyo iliyo na maskani yake Kariakoo jijini Dar es Salaam, Azim Khan, amesema hakuna timu yoyote ndogo ambayo haipendi kucheza na timu kubwa kwenye michuano yoyote ile, hivyo kwao kupangwa kucheza na bingwa mtetezi ni fahari kwao, na kutaifanya timu yao kujulikana zaidi, akiwataka mashabiki wengi wa soka kujitokeza kwa wingi kwenye mechi hiyo inayotarajiwa kucheza Januari 30, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Sisi kama Dar City, timu ambayo ipo Ligi Daraja la Kwanza na tupo kwenye nafasi za juu, tumefurahi kupangiwa na Simba, kwa sababu hakuna kiongozi wa timu yoyote ndogo asiyependa kupangiwa na timu kubwa kama Simba, Yanga au Azam, kwa sababu kuna vitu vya kujifunza kutoka kwao, lakini mechi hizo zinakuwa zinaangaliwa na watu wengi, kwa hiyo ni fursa kwetu kutangazika kama klabu na wachezaji wetu pia," alisema rais huyo.

Alisema wameshaanza kujiandaa na kujipanga kwa mchezo huo dhidi ya Simba na kwamba wapo tayari kukabiliana nayo.

"Sisi sio mchekea kama wengi wanavyodhani, mpaka tumefika hapa tumezifunga timu mbili, halafu kwenye Ligi Daraja la Kwanza nako hatufanyi vibaya," alisema.

Kwa mujibu wa droo iliyochezeshwa juzi na Shirikisho la Soka nchini (TFF), mbali na Simba kucheza na Dar City, wanafainali wa msimu uliopita, Yanga wamepangwa dhidi ya Mbao FC, na Azam FC ambayo msimu uliopita ilitolewa kwenye hatua ya nusu fainali na Simba, yenyewe itachezwa na Trasit Camp, mechi zilizopangwa kuchezwa Januari 27 hadi 31.

# Mayele atishia mastraika mbio za Kiatu

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Mkongomani Fiston Mayele amefikisha mabao sita, baada ya kufunga bao moja kwenye ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, timu yake ikiifunga Coastal Union kwenye mechi ya raundi ya 12 ya Ligi Kuu Tanzania Bara Jumapili iliyopita na kutishia mastraika hususan wazawa ambao msimu huu wanaonekana wamekuja juu.

Mayele, tayari yupo juu kwa bao moja akiwaacha mastraika wa Kitanzania wenye mabao matano kila mmoja, ambao ni George Mpole wa Geita Gold, Vitalis Mayanga wa Polisi Tanzania, Jeremiah Juma wa Prisons, ambaye kwa muda mrefu amekwama kwenye mabao hayo, licha ya kwamba mpaka sasa ndiye mchezaji pekee aliyecheka na nyavu mara tatu kwenye mechi moja 'hat-trick', na Reliants Lusajo wa Namungo.

Straika huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, huenda asikabiliane na upinzani mkubwa sana, kutokana na historia ya mastraika na wachezaji wa Kitanzania kutokuwa na mwendelezo wa kupachika mabao.

Straika Mtanzania pekee ambaye kwa zaidi ya miaka 10 alikuwa na uhakika wa kufunga angalau mabao 10 kwa msimu au zaidi ni John Bocco wa Simba, ambaye ni mshindi wa Kiatu cha Dhahabu msimu uliopita, hayuko kwenye wakati mzuri msimu huu, si tu kwamba hajafunga hata bao moja, lakini hata kiwango chake bado hakijafikia kile ambacho wengi wanakifahamu.

Hata Mkongomani mwenzake, Chris Mugalu, ambaye msimu uliopita alishika nafasi ya pili, msimu huu naye hajafunga bao lolote, akiwa ndiyo kwanza anatoka kwenye majeraha.

Inawezekana Mayele akapata wakati mgumu kutoka kwa mchezaji mwenzake wa kigeni, Meddie Kagere wa Simba raia wa Rwanda, mwenye mabao manne, ambaye ndiye anayeonekana ana mwendelezo mzuri wa kufunga.

Wachezaji wengine wenye mabao manne ni Feisal Salum wa Yanga, Juma Luzio na Richard Ng'ondya wote wa Mbeya City na Saido Ntibazonkiza wa Yanga.



Fiston Mayele

Michezo
Jumatano Januari 19, 2022
Nipashe




## Lewandowski amfunika Messi, Salah tuzo za Fifa

VUTENI SUBIRA...



Wachezaji wa Simba, John Bocco na Enock Inonga (kulia), wakiwa mazoezini. Simba itashuka Uwanja wa Manungu Jumamosi kuivaa Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

## Ushindi kuitafutia Yanga ushindi leo

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, leo watamtambulisha rasmi mchezaji wake mpya iliyomsajili kutoka TP Mazembe, Chico Ushindi, kwa kumpa nafasi kuitafutia ushindi kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha itakapocheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mbuni FC iliyoko Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Ni mechi ambayo mbali na kumtambulisha straika huyo, lakini pia wataitumia kama maandalizi ya mechi yao ya Ligi Kuu dhidi ya Polisi Tanzania inayotarajiwa kuchezwa Jumapili wiki hii kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

"Tutacheza na Mbuni FC mchezo wa kirafiki na utakuwa ni mahsusi kwa ajili ya kuwakaribisha wageni wetu wapya, mchezaji Chiko Ushindi, ambaye tumemsajili kutoka TP Mazembe, lakini kocha wa makipa Milton Nievon ambao ndiyo siku wataanza kazi rasmi na kuonekana kwa wanachama na mashabiki wetu," alisema Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli.

Wakati Chico akitokea TP Mazembe, Nievon raia wa Brazil, hivi karibuni alikuwa mmoja wa benchi la ufundi la Simba lililoondolewa na uongozi kutokana na matokeo mabaya iliyoyapata kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilipotolewa dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Kwa upande wa Mbuni FC, yenyewe mbali ya kujiandaa na mechi ya Ligi Daraja la Kwanza, lakini inajiandaa pia na mchezo wa Kombe la FA, dhidi ya Lipuli FC, mechi zinazotarajia kupigwa kuanzia Januari 29 hadi 31, mwaka huu.

# Pablo amchambua Bocco

●●●Afunguka mazito huku akiwataka mashabiki kuvuta subira, mwenyewe asema...

**Na Saada Akida**

WAKATI mashabiki wa Simba wakihoji kuhusu uwezo wa mshambuliaji wao, John Bocco, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, amemkingia kifua na kudai ni suala la muda tu kabla ya mfungaji bora huyo wa msimu uliopita kurejea katika ubora wake.

Bocco, ambaye msimu uliopita alimaliza na mabao 16, akifuatiwa na Chris Mugalu aliyefunga 15 na mshambuliaji wa Azam FC, Price Dube akimaliza na mabao 14 msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21, hadi sasa hajafunga bao hata moja kwenye ligi hiyo msimu huu huku akionyesha kiwango cha chini.

Akizungumza na gazeti hili, jana Pablo alisema Bocco ni mchezaji mzuri na kinachotokea ni kipindi cha mpito tu na kwamba anaimani anahitaji muda mfupi wa kurejea katika ubora wake.

Alisema hali hiyo inatokea kwa mchezaji kwani kuna wakati inakuwa hivyo, na anachokipitia nyota huyo hakimaanishi hajui bali ni namna ya mchezo anaokutana nao pamoja na ushindani mkubwa.

"Unakuta mchezaji anajipanga na kupania kweli kuhakikisha anafanya kile anachokitarajia katika mechi, na ikitokea akakwama inamuumiza hata yeye mwenyewe.

"Bocco ni mchezaji mzuri na ndio maana ni nahodha, nafahamu namna anavyojisikia kutokana na msimu uliopita alivyofanya vizuri, lakini sasa hajafanya vile," alisema Pablo.

Alisema anaamini kinachotokea kwa mshambuliaji wake huyo ni kipindi cha mpito kwa sababu utafika muda atarejea katika kiwango chake na kufanya vizuri zaidi.

Wakati Pablo akieleza hayo, Bocco amesema suala la kufunga ni bahati na kwamba muda ulifika na Mungu akipanga afunge atafanya hivyo.

"Kikubwa ni kuwa miongoni mwa wachezaji ambao wanacheza Simba, nikipata nafasi ninaipambania timu katika mataji yaliyobaki, mengine muda utazungumza," alisema.

Katika hatua nyingine, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, amesema kupoteza mechi dhidi ya Mbeya City, ni kuteleza na kuanguka, lakini hawalali bali wananyanyuka na kusonga mbele kwa kuwa safari bado ni ndefu.

Alisema wamepoteza mchezo wa juzi, lakini hawajapoteza malengo yao kwani yapo pale pale ya kuhakikisha wanatetea ubingwa wao.

"Tumefungwa mechi moja, lakini hatujapoteza malengo yetu yapo pale pale na tunahakikisha tunafanyia kazi kikamilifu zaidi makosa ya leo, (juzi).

"Tunateleza na kuanguka, lakini hatulali tunainuka na kusonga mbele, safari ni ndefu, ligi ina mechi nyingi tunaimani tunaenda kufanya vizuri katika mechi zijazo," alisema Rweyemamu ambaye kitaaluma ni kocha.

Simba ambayo ilipoteza juzi kwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, tayari imerejea jijini Dar es Salaam na wachezaji kupewa mapumziko ya siku moja kabla ya leo jioni kurejea mazoezini kujiandaa na mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar utakaopigwa Januari 22, mwaka huu kwenye dimba na Manungu, Tuliani mkoani Morogoro.

Licha ya kupoteza mchezo huo, bado ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi 24, nane nyuma ya Yanga inayoongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo, lakini ikiwa mchezo mmoja mbele dhidi ya watani zao hao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >